# MAJINA YA WANYAMA, NDEGE NA WADUDU YANAVYOAKISIWA NA MAJINA YA MITAA KISIWANI UNGUJA

**MWAKA MZEE MOHAMMED**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA BAADHI YAMASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (M.A KISWAHILI - ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini amethibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii yenye mada isemayo: Majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa. Ni tasnifu iliyowasilishwa kutathminiwakwa azma ya kutimiza masharti ya mahitaji ya shahada ya uzamili ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

……………………………………

**Dkt. Nestory N. Ligembe**

**(Msimamizi)**

**Tarehe………………………………**

## HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa tasnifu hii kwa njia yeyote ile bila ya idhini ya mwandishi au idhini ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi.

## TAMKO

Mimi ***Mwaka Mzee Mohammed,*** natamka kwamba kazi hii ni yangu mwenyewe haijatolewa na wala haitatolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyingine yoyote ambayo ni sawa na hii katika chuo kikuu kingine.

**……………………………………**

**Saini**

**Tarehe……………………………**

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu; Baba yangu Mzee Mohammed Khamis, Mama yangu Akama Kheir Makame, Mume wangu mpendwa Ali Mwalim Khamis, Watoto wangu Ahmed Ali, Sabra Ali, Zuhra Ali ,Haitham Ali na Ahlam Ali. Kwaniwalinisaidiakwakunipamoyo na kunivumilia katika kipindi chote cha kufanikisha kazi hii. Pia nawatabaruku wahadhiri walionifundisha na wote walionipa malezi kuanzia mwanzo hadi hapa nilipo sasa. Mwisho namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie Heri na Baraka katika maisha yetu. Amin.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na nguvu na afya njema na kuweza kufanya kazi hii ya utafiti hatimaye nimekamilisha.

Vilevile nawashukuru sana wasimamizi wangu wa utafiti Dr Nestory Ligembe na Dr Omary Muhammed kwa ushauri na msaada mkubwa mlionipa katika kazi hii ya utafiti hadi nimefikia hapa namuomba Mwenyezi Mungu awape kila la heri katika maisha yenu yote na awafungulie milango ya riziki iwe wazi kwenu, awape nguvu na afya njema.

Pia natoa shukrani zangu za dhati kwa wahadhiri wote wa idara ya kiswahili katika chuo kikuu huria Tanzania kwa namna moja ama nyingine katika suala zima la uteuzi wa mada ya utafiti, wahadhiri hao ni Dkt. Nestory Ligembe, Dkt. Zelda Elisifa, Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Hanna Simpasa na Dkt. Mohamed Omary.

Kadhalika natoa shukrani zangu za dhati kwa wazazi wangu baba yangu mzazi: Mzee Mohammed Khamis, mama yangu mzazi: Akama Kheir Makame, Pia shukrani zangu za dhati zimfikie Mume wangu Bwana Ali Mwalimu Khamis na wanangu: Ahmed Ali, Sabra Ali, Zuhra Ali, Haitham Ali na Ahlam Ali, kwa kuwa mstari wa mbele katika kunitia moyo juu ya ukamilishaji wa kazi hii. Pia walinisaidia kwa hali na mali kwa muda wote waliokuwa pamoja nami katika kazi hii adhimu,Sina budi kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awape heri na baraka, na maisha mema marefu.

Shukrani zote ziwaendee wale wote waliofanikisha utafiti huu miongoni mwao wazee na vijana wa mtaaa wa Unguja Ukuu, Ndijani, Makunduchi, Bumbwini,

Bweleo, Mkokotoni, Kitope, Kisima Majongoo pamoja navijiji na mitaa yote ambayo nimeifikia katika kufanikisha kazi yangu hi kwa kutoa mchango wao mkubwa wa kunipa data zilizo sahihi na zilizokamilisha kazi hii.

Vilevile, shukrani zangu za dhati ziwafikie wanafunzi wenzangu wa somo la Kiswahili. Ni vigumu kumshukuru kila mmoja lakini Mwenyezi Mungu atawalipa kwa kila Jambo wale wote walioshirikiana nami kufanikisha kazi hii.

# IKISIRI

Utafiti huu ulizungumzia majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanvyoakisiwa na majina ya mitaa. Ulichunguza uhusiano uliopo baina ya majina ya wanyama, ndege na wadudu. Mtafiti aliongozwa na malengo matatu. Kwanza, kubainisha majina ya wanyama ndege na wadudu yanvyotumika kuwakilisha majina ya mitaa, pili, mahusiano ya maana ya majina ya mitaa na majina ya ndege, wanyama na wadudu na tatu, kuchambua sababu zinazochangia majina ya wanyama, ndege na wadudu kuakisiwa na majina ya mitaa. Ili kufikia lengo kuu lililokusudiwa mbinu mbali mbali za utafiti zilihusika. Mbinu hizo ni pamoja na mahojiano, ushuhudiaji pamoja na hojaji. Utafiti huu uliongozwa na nadharia jumuishi pamoja na nadharia ya semiotikiambazoziliakisi data za utafiti huu kutokana na maoni yaliyotolewa na watafitiwa na wanajamii kwa ujumla, ambapo maoni hayo yaliunda data za utafiti huu. Kwa upande wa matokeo ya utafiti, mtafiti aligundua kuwa majina ya mahali yana mfungamano na jamii na utamaduni wa jamii husika. Baadhi ya majina yanaakisi moja kwa moja shughuli za kiuchumi ama kijamii wanazofanya wanajamii. Hata hivyo, kuna majina ya mitaa ambayo hutokana na matendo ya kihistoria yaliyofanywa na wakazi wa maeneo hayo.Sambamba na hayo mtafiti katika kazi yake amegundua pengo ambalo linahitaji kufanyiwa kazi, ambapo anapendekeza kufanyika kwa utafiti utaonesha athari za majina ya viumbe, vitu pamoja na matendo ya watu jinsi yanavyoakisi katika utoaji wa majina ya mitaa. Na pia athari za kifonojia, kimofolojia na kisemantikia vifanyiwe utafiti ili kuweza kuona jinsi gani wanajamii wanavyoweza kuvitawala vyema vipengele vya kiisimu katika utoaji na upangaji wa majina ya sehemu wanazoishi maishani.

# YALIYOMO

UTHIBITISHO ........................................................................................ i

HAKIMILIKI ........................................................................................ ii

TAMKO.. ........................................................................................ iii

TABARUKU ........................................................................................ iv

SHUKRANI ........................................................................................ v

IKISIRI.. ........................................................................................ vii

YALIYOMO ........................................................................................ viii

ORODHA YA MAJEDWALI ........................................................................................ xiii

**SURA YA KWANZA ........................................................................................ 1**

**UTANGULIZI ........................................................................................ 1**

1.1 Utangulizi ........................................................................................ 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........................................................................................ 1

1.3 Tamko la tatizo la utafiti ........................................................................................ 4

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................................ 5

1.4.1 Lengo Kuu ........................................................................................ 5

1.4.2 Malengo Mahsusi ........................................................................................ 5

1.5 Maswali ya Utafiti ........................................................................................ 6

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................ 6

1.7 Mpangilio wa Tasnifu ........................................................................................ 7

1.8 Mipaka ya Utafiti ........................................................................................ 7

1.9 Vikwazo vya Utafiti ........................................................................................ 8

1.10 Maadili ya Utafiti ........................................................................................ 9

1.11 Muhutasari wa Sura ........................................................................ 9

**SURA YA PILI ........................................................................................ 10**

**MAPITIO YA MAANDIKO NA NADHARIA YA UTAFITI ........................... 10**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 10

2.2 Mapitio ya kazi tangulizi kinadharia (Theoretical Literature Review) ....... 10

2.2.1 Dhana ya Kihistoria kuhusu Mitaa ........................................................ 10

2:2.2 Dhana kuhusu Utoaji wa Majina ............................................................ 12

2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Kitafiti (Emprical Litrature Review) ........... 14

2.3.1 Kazi Tangulizi za Kitafiti zilizozungumzia Majina ya Mahali na Mitaa .... 14

2.3.1.1 Kazi Tangulizi za kitafiti zilizozungumzia Majina ya Mahali ................... 15

2.3.1.2 Kazi Tangulizi za kitafiti zilizozungumzia Majina ya Mitaa Tanzania ...... 16

2.3.2 Kazi Tangulizi za Kitafiti zilizozungumzia Mahusiano ya Maana ya majina ya Mahala na Mitaa ........................................................ 17

2.3.2.1 Tafiti Tangulizi zilizoangazia Mahusiano ya Kimaana katika Majina ya mahala ........................................................................ 17

2.3.2.2 Tafiti Tangulizi zilizoangazia Mahusiano ya Kimaana katika Majina ya Mitaa ........................................................................ 19

2.3.3 Kazi Tangulizi za Kitafiti zilizozungumzia sababu zinazochangia katika Utoaji wa Majina ya Mahala na Mitaa ...................................................... 21

2.3.3.1 Kazi tangulizi za kitafiti zilizozungumzia Sababu zinazochangia katika Utoaji wa Majina ya Mahala ................................................................ 21

2.3.3.2 Kazi tangulizi za kitafiti zilizozungumzia sababu zinazochangia katika Utoaji wa Majina ya Mitaa au Vijiji ........................................................ 22

2. 4 Pengo la Kiutafiti ........ 25
2.5 Kiunzi cha Nadharia ........ 25
2.5.1 Nadharia ya Semiotiki ........ 26
2.5.2 Nadharia Jumuishi ........ 28
2.6 Muhutasari wa Sura ........ 29

**SURA YA TATU ........ 30**

**MBINU ZA UTAFITI ........ 30**

3.1 Utangulizi ........ 30
3.2 Eneo la utafiti ........ 30
3.3 Mkabala wa Utafiti ........ 31
3.4 Walengwa wa Utafiti ........ 32
3.4.1 Sampuli na Usampulishaji ........ 32
3.4.2 Usampulishaji Lengwa ........ 34
3.5 Aina za Data ........ 34
3.5.1 Data za Maktabani ........ 34
3.5.2 Data za Uwandani ........ 35
3.6 Mbinu za Kukusanyia Data ........ 35
3.6.1 Mbinu ya Hojaji ........ 36
3.6.2 Mbinu ya Mahojiano ........ 36
3.6.3 Mbinu ya Ushuhudiaji ........ 37
3.7 Vifaa vya Utafiti ........ 37
3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data ........ 38
3.9 Uwasilishaji na Uchambuzi wa data ........ 38

3.10 Muhutasari wa Sura ..... 39

**SURA YA NNE ..... 40**

**UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI .. 40**

4.1 Utangulizi ..... 40

4.2 Majina ya Wanyama ndege na Wadudu Yanavyowakilisha Majina ya Mitaa ..... 41

4.2.1 Uteuzi wa Jina la mtaa wa Kiziwa Ndege ..... 42

4.2.2 Uteuzi wa jina la mtaa wa Kisima Ng'ombe ..... 44

4.2.3 Uteuzi wa jina la mtaa wa Mwembe Majogoo ..... 46

4.2.4 Uteuzi wa jina la mtaa wa Mwembe Punda ..... 49

4.2.5 Utoaji wa jina la Mtaa wa Kiunga Ndege ..... 51

4.2.6 Uteuzi wa Jina la mtaa wa Kicheche ..... 53

4.2.7 Uteuzi wa Jina la Mtaa wa Mwembepopo ..... 55

4.2.8 Uteuzi wa Jina la Mtaa wa Kisima Majongoo ..... 57

4.2.9 Uteuzi wa jina la Mtaa wa Mlandege ..... 59

4.3 Mahusiano ya Maana ya Majina ya Mitaa na Majina ya Wadudu, Wanyama na Ndege ..... 59

4.3.1 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kiziwandege ..... 60

4.3.2 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kisimang’ombe ..... 61

4.3.3 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Mwembemajogoo ..... 61

4.3.4 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Mwembepunda ..... 62

4.3.5 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kiungandege ..... 62

4.3.6 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kicheche ..... 63

4.3.7 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Mwembepopo ............................ 64

4.3.8 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kisimamajongoo........................ 64

4.3.9 Mahusiano ya kimaana ya jina la Mtaa wa Mlandege ............................... 65

4.4 Sababu Zinazochangia Majina ya Wanyama, Ndege na Wadudu Kuakisiwa na Majina ya Mitaa ........................................................................ 66

4.5 Muhutasari wa Sura ...................................................................... 67

**SURA YA TANO ........................................................................ 68**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................ 68**

5.1 Utangulizi........................................................................................ 68

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .................................................. 68

5.2.1 Matokeo ya lengo la kwanza la utafiti ........................................ 69

5.2.2 Matokeo ya Lengo la pili la Utafiti............................................ 70

5.2.3 Matokeo ya lengo la tatu la utafiti ............................................ 70

5.3 Mapendekezo juu ya Tafiti Zijazo ................................................ 71

5.4 Muhutasari wa Sura ...................................................................... 72

**MAREJELEO ................................................................................ 73**

**VIAMBATANISHO ........................................................................ 77**

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali na.3.1: Linaonesha sampuli ya Watoa Taarifa............................................. 33

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii ilihusisha sehemu ndogo ndogo ambazo ni usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mpangilio wa tasnifu, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti maadili ya utafiti na muhtasari.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Majina ni utambulisho ambao ni tahajia yamajina ya watu, vitu, wanyama, mimea na hata pahala. Masamba (2004) anasema kuwa; Jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbe hai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, maarifa au tukio katika tungo. Naye Nigro (2015) ameeleza kuwa majina yana maana ya upekee (anomalstics or anomatology) na yanachukua nafasi ya kila kitu ambapo hujumuisha majina ya pahali (toponyms) na majina ya watu (anthroponyms). Kutokana na dhana hizo basi tunasema kuwa majina ni utambulisho ambao hutambulisha watu, vitu pamoja na mahali. Pia majina ya mitaa hutolewa kwa mujibu wa matokeo ya kihistoria, kuhifadhi na kulinda utamaduni wa jamii husika, kuenzi na kukumbuka mchango wa viongozi au watu mashuhuri katika nchi au Taifa husika.Sambamba na hayo wataalamu mbalimbali wanatueleza kuwa utoaji wa majina ya mahala au mitaa kwa kiasi kikubwa hutokana na kuhifadhi pamoja na kulinda historia, mila na utamaduni wa jamii husika, {Funk 1997, Muzale 1998na Msanjila na wenzake 2009). Hata hivyotunaweza kuona kuwa kuna aina tofauti za majina ambayo yakiwemo majina ya pekee, ambayo hujumuisha majina ya watu, miji, maziwa, nchi na hata vijiji, majina hayo ni pamoja na: Matyas, Eliza Tanzania, Kenya, Geita,

Arusha. Vile vile kuna majina ambayo hurejelea dhanambalimbali kama vile vitu au viumbe hai mfano:jina “kiti” hurejelea kifaa cha kukalia au nyadhifa fulani katika uongozi, hata hivyo jina“kisu” nalo hurejelea kifaa cha kukatia. Pamoja na hayo kuna majina ya dhahania ambayo hufikirika tu na maranyingi majina kama haya huwa hayana umbo maalum katika uwakilisho wake na hivyo huwa hayaonekani kwa macho kile kinachowakilishwa na majina hayo bali huwepo na kutumiwa kutokana na makubaliano ya kijamii tu na kubaki akilini mwa watumiaji wa lugha husika mfano wa majina hayo ni kama vile usingizi, utamu, ukali na hasira. Vile vile kunamajinaambayohuwakilishadhana fulanikimakundi (majina ya jamii) ambayo hutaja kitu kimoja tu lakini ndani yake huwakilisha vitu zaidi ya kimoja hii ni kutokana na kuwa vitu hivyo vinajumuisha sifa za aina moja mfano timu, vyombo, bunge, ndege na wanyama. Hivyo, tunapoangalia majina ya ndege na wadudu pamoja na wanyama ni majina yanayopatikana katika majina ya makundi (majina ya jamii), kwani ndani ya aina hiyo kuna ndege wa aina tofauti ambao wameweza kuwekwa katika kundi la ndege kutokana na kuchangia sifa zinazofanana, halikadhalika kwa wadudu na wanyama ambao ndani yao kuna aina tofauti. Na kwa upande wa majina ya mitaa nayo yamejikita katika majina ya pekee ambamo hupatikana majina ya sehemu, vitongoji au vijiji tofauti kutokana na historia, matendo au hulka za wakaazi wa jadi katika eneo husika. Hivyo basi majina ya viumbe hivyo yana mchango mkubwa katika uteuzi wa majina ya mitaa.

Ingawaje, majina ya mitaa huteuliwa kutokana na sababu mbali mbali zinahusiana na eneo husika zikiwemo, kulinda utamaduni au kuthamini mchango wa viongozi wa juu, kama ambavyo ilivyojitokeza katika uteuzi wa jina la Kiwanja cha ndege cha

Karume, uwanja wa mpira wa Mausitung, barabara ya Mkapa, Kasri ya mwinyi mkuu pamoja na mtaa wa Nyerere ambayo inapatikana katika kisiwa cha Unguja. Hivyo, majina hayona yaliyofana na hayo hupewa majina yao kutokana na matendo na harakati za kibinaadamu zitakazokuwa zinafanyika kulingana na mazigira yaliyomzunguka. Hata hivyo, uteuzi wa majina kijamii hufanywa kwa lengo lakutofautisha jamii moja na nyigine kutokana na umbali wa kijografia uliopo baina ya jamii moja na nyingine. Tukiendelea zaidi, majina yamitaa yanamchango mkubwa katika kukuza tamaduni pamoja na kutambulisha asili za jamii husika.Kama vile kuna jamii ya Wazaramo na Wahehe namila zao (Mgulu 2002, Matinde 2012 pamoja na Massamba 2004).

Sambamba na hayo majina huundwa kwa michakato mbali mbali ya kimofofonolojia ambayo huleta mabadiliko ya kimofofonolojia yenye kubeba ufafanuzi wa kifonetiki. Mabadiliko hayo hutokea pale ambapo sauti mbili zinapoathiriana katika mazingira ya utokeaji wao katika umbo la ndani la jina husika na wakati wa kulitamka ama kuliandika katika umbo la nje hupokea mabadiliko, hii ni kutokana na kuwepo kwa michakato ya kimofofonolojia. Kwa minajili hiyo, Wanaisimu wameyafanyia uchunguzi wa kina mabadiliko hayo na kuunda kanuni mbalimbali ambazo ziwe ni miongozo katika kuonesha ukokotoaji wamaumbo ya ndani kwenda ya nje. Hivyo katika dhana ya uteuzi wa majina ya mitaa muathiriano wa namna hiyo huweza kujitokeza na kulibadilisha jina na kupokea sura mpya ya kimatamshi ama kimaandishi kutokana na umbo la ndani la jina kufanyiwa michakato hiyo wakati wa kupelekwa umbo la nje.

Hivyo basi, mtafiti amekusudia kufanya utafiti ambao unahusiana na majina ya wanyama ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa, pamoja na kuangazia michakato ya kimofofonolojia ambayo imetumika katika unasibishwaji wa majina ya wanyama, ndege na wadudu katika utoaji wa majina ya mitaa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mtafiti ameona kuwa kuna mwanya mkubwa wa kitaaluma ambao unahitaji kuzibwa kupitia kazi ya kitafiti.

## 1.3 Tamko la tatizo la utafiti

Utafiti huu ulionesha majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa. Majina ya mitaa ni utambulisho unaotambulisha na kutofautisha baina ya mtaa mmoja na mwengine. Watafiti mbali mbali wameangalia utoaji wa majina huku wakiangazia sababu, mila, desturi na hata tamaduni za jamii ya mitaa husika. Miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na Njozi (2010) aliangazia asli na sababu za jina la Mwembe kunyonga na aligundua kuwa chanzo cha kuwepo jina hilo ni kutokana na matendo ya kihistoria ya mauwaji yaliyokuwa yakifanyika Kilwa, na hapo ndipo likaibuka jina hilo. Naye Abeid (2005) alichapisha jarida ambalo linahusiana na majina ya mitaa na kusema kuwa kila mtaa hupewa jina kutegemeana na historia iliyotokea ama iliyopita, vituko /vioja, vitakavyokuwa vinafanywa na watu wanaoishi katika eneo husika, ubabe ama kufananishwa na tabia za wanyama au tukio ambalo linafanana na wakaazi wa mtaa husika. Kama vile mtaa wa Jang'ombe amedai kuwa mtaa huu watu wake wana tabia za King'ombe ng'ombe hata hivyo aliendelea kueleza kuwa jina la mtaa wa Regezamwendo nalo linatokana na tabia za watu kupunguza mwendo wanapofika eneo hilo kutokana na mlima uliokuwepo hapo. Kwa upande wa Schotsman (2003) yeye alitafiti kuhusu majina ya

vituo vya dala dala na mitaa ya Dar es Salaam, katika tafiti yake hiyo alieleza kuwa majina ya mitaa yanatokana na sababu, historia ya eneo husika na ipo mitaa mengine hupewa majina kutokana na harakati za kuwaenzi viongozi mashuhuri kutokana na kuithamini michango yao katika kulitetea Taifa majina hayo ni kama vile Kawawa, Mawese na Mwananyamala.

Pamoja na kwamba wataalamu wengi waliangalia majina ya mitaa kwa kusema, majina mengi hutokana na sababu, historia mila na hata utamaduni wa jamii husika lakini hakuna machapisho ama tafiti yeyote ile ambayo imeangazia majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa. Kwa muktadha huo mtafiti ameshawishika kufanya utafiti katika eneo hilo pamoja na kuangalia michakato ambayo hujitokeza katika utoaji na upangaji wa majina ya mitaa.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti yamegawika katika makundi makuu mawili: lengo kuu na malengo mahsusi

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa kisiwani Unguja.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahususi ya utafiti huu, ni haya yafuatayo:

i) Ubainishaji wa majina ya wanyama, ndege na wadudu yanayotumika

kuwakilisha majina ya mitaa kisiwani Unguja.

ii) Kubainisha mahusiano ya maana majina ya mitaa na majina ya wadudu, wanyama na ndege kisiwani Unguja.

iii) Kuchambua sababu zinazochangia majina ya mitaa kuakisiwa na majina ya wanyama, ndege na wadudu kisiwani Unguja.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

1. Ni majina yapi ya wanyama, ndege na wadudu yanayotumika kuwakilisha majina ya mitaa kisiwani Unguja?
2. Kwa nini majina ya wanyama ndege na wadudu huakisiwa na majina ya mitaa?
3. Sababu zipi zinazochangia majina ya mitaa kuakisiwa na majina ya wanyama, ndege na wadudu?

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ukikamilika utawasaidia wanafunzi walimu na wasomi katika nyanja tafauti za kitaaluma na kijamii katika kupanua uwelewa zaidi kuhusu majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa.

Utafiti huu utatoa mchango katika nyanja ya isimu hasa taaluma ya isimu jamii kwa kuonesha uhusiano uliopo katika majina baina ya wanyama, ndege na wadudu namna yanavyoakisiwa na majina ya mitaa.

Utafiti huu utasaidia jamii kufahamu historia na matukio muhimu ambayo yanahusiana na mitaa ambayo yanachangia kuzuka kwa majina ya mitaa hiyo.

Utafiti huu utasaidia kukuza msamiati wa lughakutokana na kuongezeka majina ya wanyama, ndege na wadudu ambayo wanajamii walikuwa hawaelewi jinsi majina hayo yanavyoweza kuibua majina ya mitaa kwa kuzingatia sifa, tabia hasi au chanya za viumbe hivyo.

Utafiti huu utatoa mchango kwenye nyanja ya taaluma ya isimu kama marejeleo ya fani hiyo kwa kuonesha jinsi lugha inavyotumika kuitambulisha jamii.

Ingawaje utafiti huu umelenga katika isimu lakini pia utasaidia katika nyanja ya taaluma ya fasihi kwani jamii itaweza kuona historia halisi za majina ya wanyama ndege na wadudu jinsi wanavyoweza kuibua majina ya mitaa kwa kuzingatia sifa,tabia pamoja na harakati za kijamii na kiuchumi.

Utafiti huu utasaidia kuibua maeneo zaidi ya utafiti wa utafutaji wa majina mengine ambayo yanahusiana na mitaa.

## 1.7 Mpangilio wa Tasnifu

Tasnifuhii ina sura tano. Sura ya kwanza itahusu utangulizi wa jumla. Sura ya pili ni mapitio ya kazi tangulizi pamoja na nadharia iltakayotumika katika utafiti huu. Sura ya tatu ni mbinu za utafiti zitakazotumika katika utafiti huu. Sura ya ya nne ni uwasilishaji na uchambuzi wa data zitakazopatikana katika utafiti. Sura ya tano itatoa muhtasari wa utafiti, hitimisho na mapendekezo.

## 1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuangalia majina ya wanyama, ndege nawadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa. Mtafiti alifanya utafiti wake katika kisiwa cha

Unguja,ndani ya Mikoa mitatu yenye Wilaya Saba (7) kupitia Wilaya hizo mtafiti alikuwa na uhakika wa kupata data zinazohusiana na tatizo la utafiti husika, kutokana na ukaribu wa maeneo ambayo mtafiti ameyafikia katika ukamilishaji wa kazi yake.Hata hivyo watafitiwa ambao mtafiti aliwatafiti walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusiana na majina ambayo mtafiti aliyashughulikia katika kazi yake.

### 1.9 Vikwazo vya Utafiti

Katika utafiti huuvikwazo mbalimbali vilijitokeza, hata hivyo mtafiti alipambana navyo na kuvitafutia ufumbuzi, vikwazo hivyo ni pamoja na:

Kukutana na watu ambao kwa mara ya kwanza kukutana nao na kutaka taarifa zinazohusiana na mitaa yao, ambapo watu hao walipinga kutoa taarifa hizo kwa vile ilikuwa hawana taaluma ya kufanya hivyo kwa vile baadhi ya watoa taarifa walilihusisha suala hili na imani za kishirikina na wapo ambao walilihusisha suala hili na kasumba za kisiasa.

Pamoja na hayo watafitiwa wa utafiti huu wengi wao walikuwa ni watu wazima ambao wamekosa taaluma ya kusoma na kuandika na hivyo ikamlazimu mtafiti atumie mbinu ya mahojiano pamoja na ushuhudiaji zaidi kuliko mbinu ya hojaji ili kupata data zilizomuwezesha mtafiti kuyafikia na kuyakamilisha malengo ya utafiti wake.

Sambamba na hayo mtafiti alikumbana na kikwazo cha usafiri cha kutoka Wilaya hadi Wilaya, Mkoa hadi Mkoa na wakati mwengine kukosa usafiri kabisa na kumfanya alazimike kukodi boda boda ili aweze kufika katika maeneo teule na

kujipatia data zilizoweza kukamilimilisha malengo matatu ya utafiti wake.

### 1.10 Maadili ya Utafiti

Mtafiti amezingatia maadili ya kiutafiti kwa kuwa muwazi kwa walengwa, kuwasilisha data na matokeo kwa usahihi na uaminifu kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti.Aidha taarifazilizopatikana kutoka kwa watafitiwa zilitumika kwa ajili ya utafiti tu na si vyenginevyo. Mtafiti ameweka wazi taarifa za watafitiwa bila ya kutaja majina yaokwa lengo la kuwalinda na kuwahifadhi. Hata hivyo, mtafiti katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data zake amezingatia maswali yaliyo lenga moja kwa moja mada ya utafiti, alizingatia muda wa kuanza na kumaliza zoezi zima la ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti husika, sambamba na hayo mtafiti alizingatia faida na umuhimu wa utafiti kwa watu wa jinsia na tabaka zote katika jamii.Pamoja na yote mtafiti ameepukana na kosa la kunakili kazi za watu(Plagarisms) bila kuwataja na kujielimisha kwa kufuata sheria za nchi katika kufanya utafiti.

### 1.11 Muhutasari wa Sura

Sura hii ilihusu utangulizi wa jumla kuhusu vipengele mbalimbali vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu. Vipengele hivyo ni utangulizi, usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mpangilio wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti pamoja na maadili ya utafiti. Sura inayofuata inahusu mapitio ya maandiko na nadharia ya utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA NADHARIA YA UTAFITI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii iliangazia sehemukuu mbili. Sehemu ya mapitioyamaandiko ya kazi tangulizi za wataalamu mbalimbali. Maandiko ya kazi tangulizi hizo zilizoangaziwa katika tafiti hii ni pamoa na zile zilizohusiana kwa namna moja au nyingine na mada ya utafiti. Mtafiti amepitia maandiko ya kazi tangulizi hizo za wataalamu waliotangulia kwa lengo la kupata taarifa mbalimbali zilizohusiana na utafiti huu. Taarifa hizi ziliweza kumsaidia mtafitina kubainisha pengo la utafiti ambalo aliweza kulifanyia utafiti wake. Sehemu ya pili ya sura ilieleza nadharia zilizotumika katika utafiti huu, ambazo ni nadharia ya semiotiki pamoja na nadharia jumuishi na mwisho kuishia na muhutasari wa sura.

## 2.2 Mapitio ya kazi tangulizi kinadharia (Theoretical Literature Review)

Mtafiti amepitia mapitio ya kazi tangulizi tofauti zilizohusiana na tatizo la utafiti kazi hizo zimegawanywa kupitia vipengele vifuatavyo:

### 2.2.1 Dhana ya Kihistoria kuhusu Mitaa

Mitaa ni dhana iliyozoeleka kutokana na historia ya watu au vitu miongoni mwa wanalugha wajamii mbalimbali zilizoishi katika maeneo tofauti duniani kote. Historia ya majina ya mitaa ni kipengele muhimu sana katika kuhifadhi utamaduni na utambulisho wa eneo fulani au hata tukio lililowahi kutokea katika maeneo ambayo wanaadamu huishi. Kipengele cha majina ya mitaa kimezungumzwa nawataalamu mbalimbali duniani kote, katika kukitolea ufafanuzi pamoja na kukifanyia tafiti mbalimbali na kukiandalia vitabu, makala pamoja na tasnifu

mbalimbali kuhusu uwanja wa historia ya mitaa. Wataalamu waliozungumzia historia ya mitaa, ni pamoja na:

Abeid (2005) aneleza kuwa kila tukio huacha athari sehemu hiyona kuifanya kuwa ni historia. Akithibitisha hili Abeid (keshatajwa) anaifafanua dhana ya mitaa kuwa huendana nautamaduni wa jamii ya pale ulipo mtaa husika, na hujulikana kwa vituko, viroja[1], uimara, ubabe na usumbufu wa mitaa na watu wanaoishi hapo. Akitolea mfano katika makala inayoelezea dhana ya Magofu ya watawala wa jadi Abeid (ameshatajwa) ametaja baadhi tu ya mitaa kama vile: *Jang`ombe, Mwera na Regezamwendo* na kuihusisha mitaa hiyo na tabia hasi au chanya za kihistoria kulingana na wakaazi wake na matendo yao. Naye Juma (2010) anakubaliana na Abeid (ameshatajwa) kwa kudai kuwa historia ya majina ya mitaa ipatikanayokisiwani Unguja inatokana na tabia na ujasiri waliokuwa nao watawala wa jadi walioishi katika maeneo husika, sambamba na hayo Juma(ameshatajwa) analithibitisha hili kwa kutaja baadhi ya majina ya mitaa kama: Fukuchani na Bungi. Hivyo basi, tunaungama na mawazo ya wataalamu wote hao, na hivyo kazizao hizi ni muhimu sana katika tafiti yetu hii kwa vile zilimuwezesha mtafiti kupata mbinu na njia mbali mbali zilizomsaidia katika kuchunguza historia ya majina ya wanyama,wadudu na ndege jinsi yanavyoakisiwa na utoaji wa majina ya mitaa kisiwani Unguja.

[1] Ni aina ya visa mbalimbali ambavyo mtu huamua kufanya ili kumkimbiza mtu ambaye ama hapendi kuwa naye karibu au kujua shida zake.

### 2:2.2 Dhana kuhusu Utoaji wa Majina

Wataalamu mbalimbaliulimwenguni kote hawakuwa nyuma katika kuelezea utoaji wa majina. Miongoni mwa wataalamu hao ni(Funk 1997;Muzale 1998;Msanjila 2009).

Funk (1997) anaeleza kuwa, mchakato wa utoaji wa jina huelezea mengi kuhusu mwanaadamu na jinsi anavyohusiana na ulimwengu unaomzunguka. Akilithibitisha hili Funk (ameshatajwa) anasema utoaji wajina ni tendo kama matendo mengine, ambalo limo katika muktadha wa kisiasa, hivyo kuita kitu au mtu ni tukio la kisiasa. Funk (ameshatajwa) akiendelea kufafanua zaidi, anadai kuwa utoaji wa majina ya namna hii unaweza kuibua masuala ya mtu mmoja mmoja na hata ya kijamii, pia akiendelea kusisitiza kuwa utoaji wa majina huo kwa mtu mmoja mmoja au jamii bado hujaweza kuibainisha na kuipambanua jamii moja na nyingine. Naye Guma (2001) akiunga mkono dai la Funk (ameshatajwa) kwa kusema kuwa, mchakato wa utoaji wa majina ni tukio la kijamii pamoja na kiutamaduni lenye kuonesha historia ya jamii husika, vile vile majina hayo husimamia tajriba ya mtu au kikundi cha watu, mila, desturi, hadhi na mamlaka katika jamii husika. Kwa minajili hiyo tunakubaliana na wataalamu wote hawa kwa vile utoaji wa majina hubeba utambulisho wa jamii husika kama ambavyo majina ya ndege, wanyama na wadudu yanavyo akisiwa na majina ya mitaa pamoja na kuitambulisha mitaa hiyo katika jamii nyingine.

Hivyo kazi za Guma na Funk zote zilitoa mwanga wa kitaaluma kwenye tafiti yetu hii, kwa vile zilimsaidia mtafitikinadharia pamoja na kuchunguza jinsi utoaji wa

majina ya mitaa yanavyohusiana na historia pamoja na mazingira  kulingana na harakati za kimaisha za mwanaadamu.

Naye Muzale (1998) anaeleza kwamba kutoa jina ni kutoa maana. Majina ya binaadamu yanaweza kutusaidia kuwa na mkabala mwengine katika Isimu jamii na isimu historia na kujifunza vipengele vya kihistoria na kijamii katika jamii husika. Maelezo hayo, ya Muzale (ameshatajwa) yanatubainishia kwamba, majina ni kipengele muhimu katika kuelezea masuala yanayohusu jamii na historia ya jamii husika, kwa vile jina huwa ni sehemu ya utambulisho wa jamii hiyo hii ni kutokana na kuwa katika uteuzi na upangaji wa jina kuna kuwa na mambo kadhaa yanayoakisi jina hilo litokee kama lilivyo, hasa majina yanayotolewa katika jamii mbalimbali za kiafrika. Pamoja na hayo Muzale (ameshatajwa) akitilia mkazo hili anadai kuwa utoaji wa jina huenda sambamba na matukio ya kihistoria na amali za jamii husika. Hata hivyokazi hii ni muhimu kwani imetupatia maarifa ya kitaaluma yanayohusu mbinu mbalimbali zitumiwazo na watu katika utoaji wa majina ya mitaa.

Msanjila na wenzake (2009) wamezungumzia kuhusu umuhimu wa majina. Katika ufafanuzi wao, wameelezeakuhusu mahusiano katiya majina na familia, vitu pamoja na matukio muhimu katika jamii. Hata hivyo, Msanjila na wenzake (wameshatajwa) katika kazi yao hiyo wanatueleza kuwa majina mengi yanayotolewa hutolewa kwa lugha inayozungumzwa na jamii husika, na kubeba maana inayotokana na utamaduni wa mazingira ya jamii hiyo na hapo ndipo majina hayo yanapo eleweka kwa wanajamii wenyewe kwavile  wanachukuliwa kuwa  wanamaarifa, elimu na uzoefu katika maisha yanayofanana baina yao.Msanjila na wezanke (wameshatajwa) wanafafanua zaidi kuhusu maana za majina, kwa kusema kuwa  majina huweza

kubeba maana kutokana nauhusiano wa kiutamaduni katika mazingira ya wazungumzaji, tabia ya jamii iliyopo, mapito ya misimu na mabadiliko ya nyakati na siku pamoja na utokeaji wamatukio ya kihistoria yanayo husu jamii husika.

Kwa mantiki hiyo ni kwamba, kazi hii inaumuhimu mkubwa sana katika tafiti yetu hii kwani imemuwezesha mtafiti kubaini sababu za msingi zitumikazo katika utoaji na upangaji wa majina kiujumla pamoja na kumpatia fursa adhim mtafiti katika kulibaini ombwe la kiutafiti ambalo linahitaji kufanyiwa utafiti wa kina kuhusu majina ya wanyama, ndege na wadudu yanavyotumika kama kipengele cha utambulisho na jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa

## 2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Kitafiti (Emprical Litrature Review)

Watafiti mbalimbali duniani kote walitafiti kuhusu dhana yamajina ya mahala au mitaa kwa kuyalinganisha, kutafuta sababu za uwepo wao pamoja na kuangalia vigezo mbalimbali vinavyotumika katika uteuzi wa majina hayo, kihistoria, mila pamoja na mazingira husika. Hivyomtafiti ameangazia kazi mbali mbali zikiwemo kazi zilizotafitiwa Barani Ulaya, Asia, Amerika, Afrika kwa ujumla wake, kazi hizo zinawiana kwa namna moja au nyingine na mada ya utafiti husika na mtafiti amezibainisha kazi hizokama ifuatavyo:

### 2.3.1 Kazi Tangulizi za Kitafiti zilizozungumzia Majina ya Mahali na Mitaa

Wataalamu mbalimbali duniani kote ikiwemo Ulaya, Amerika, Asia na Afrika, hawakuwa nyuma katika kutafiti majina ya mahali yanavyowakilishwa na vitu au matukio yatokanayo na jamii husika. Miongoni mwa wataalamu hao ni kama inavyodhihirishwa katika 2.3.1.1 pamoja na 2.3.1.2.

#### 2.3.1.1 Kazi Tangulizi za kitafiti zilizozungumzia Majina ya Mahali

Watafitimbalimbali ambao wametafiti kuhusu majina ya mahala miongoni mwao ni pamoja na: Roden (1974) alitafiti kuhusu majina ya mahala katika nchi ya Uganda. Katika utafiti wake huo alibaini kuwa majina ya mahala yanaonesha maana mbalimbali zinazotokana na utambulisho wa mtu mmoja mmoja, uhusiano wa kifamilia au hadhi ya kazi inayofanywa na mtu husika. Tunaungana na Roden (ameshatajwa) pale aliposema kuwa majina ya mahala huonesha maana zitokanazo na utambulisho wa mtu, familia au kazi kwani hata baadhi ya majina ambayo yaliyonasibishwa na majina ya ndege, wanyama na wadudu mengi yao yalitokana na utambulisho, uwepo wao na hata harakati za kiutamaduni zilizokuwa zikifanyika kipindi fulani cha maisha waliopitia wakaazi wa eneo husika kama ambavyo tatizo la utafiti linavyojieleza.

Naye Rey (1995) alitafiti kuhusu majina yanayotambulisha watu au mahali katika jamii tofauti. Matokeo ya utafiti huo, unaonesha kuwa kuna utofauti kubwa baina ya jamii moja na nyingine kutokana na vigezo vya asili, historia na utamaduni.Kutokana na maelezo ya Rey (ameshatajwa), tunakubaliana naye kwakusema kuwa utambulisho wa majina ya watu au mahala hutofautiana kutokana na vigezo vya asili, kihistoria na hata utamaduni, kwa vile hata majina ya mitaa ambayo huwakilishwa na kunasibishwa na majina ya wanyama, ndege na wadudu mengi yao hutolewa kwa kuangalia asili, historia na hata matukio ya kiutamaduni ambayo yatakuwa yanafanywa na jamii husika itakayokuwa inaishi katika eneo husika.

Hivyo basi, kazi za wataalamu hawa Rey na Roden (wameshatajwa) zilikuwa muhimu na zilitusaidia katika kuyafikia malengo yetu mawili ya utafiti huu likiwemo

lengo la kwanza ambalo lililenga ubainishaji wa majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanayotumika kuwakilisha majina ya mitaa, pamoja na lengo la tatu nalo lililenga kuchambua sababu zinazochangia majina ya mitaa kuakisiwa na majina ya wanyama, ndege na wadudu. Kwa vilewatafitiwa wa kazi hizo wameonesha kuwa majina ya mahala hutolewakwa kuangalia utambulisho, au hadhi ya mtu mmoja na mwengine, asili, historia nahata utamaduni wa jamii husika.

#### 2.3.1.2 Kazi Tangulizi za kitafiti zilizozungumzia Majina ya Mitaa Tanzania

Watafiti mbalimbali wametafiti kuhusu majina ya mitaa miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na: Seif (2011) alifanya utafiti kuhusiana na asili ya majina ya mitaa iliyopo Morogoro. Na matokeo ya utafiti wake huo yanaonesha kuwa majina hayo yanatokana na vitu pamoja na asili ya matendo mbalimbali yaliyokuwa yakifanywa na wakaazi wa mitaa husika. Akitoa mifano ya mitaa hiyo ni pamoja na mtaa wa “Gairo” ambapo anatueleza kuwa mtaa huu asili yake ni “*Kigairo*” yaani sehemu ya kugawiana vitu, kutokana na kuwa hapo zamani watemi walilitumia eneo hilo kwa kugawiana meno ya ndovu, pamoja na hayo anadai kuwa Wakaguru walikuwa wanasema “*Chikututa chigairo*” yaani wanamaanisha kuwa wanakwenda sehemu ya kugawiana. Baadae likawa "*Gulio*" likimaanisha soko la jumla na reja reja.Hata hivyo, Seif (keshatajwa) aliendelea kudai kuwa “Msingisi”ni jina linalotokana na mto wa Kikaguru unaoitwa msingisi. Kwa mintarafu hiyo, utafiti huu ni muhimu sana na umemsaidia mtafiti katika kazi yake kugundua na kubaini vigezo na matukio mbalimbali yatokeayo katika jamii na jinsi yanavyotumika katika kuakisi uteuzi wa majina ya mitaa kiasili na kihali.

### 2.3.2 Kazi Tangulizi za Kitafiti zilizozungumzia Mahusiano ya Maana ya majina ya Mahala na Mitaa

Wataalamu mbalimbali ulimwenguni walifanya tafiti mbalimbali zilizoangazia mahusiano ya kimaana katika majina ya mahala na mitaa, katika tafitii hizo majinayaliyochunguzwa mengi yao yalihusishwa kimaana kupitia vipengele vya kihistoria na kiutamaduni, miongoni mwa watafiti waliotafiti tafiti zinazohusu majina na maana ni pamoja na hawa katika 2.3.2.1 pamoja na 2.3.2.2 hapa chini:

#### 2.3.2.1 Tafiti Tangulizi zilizoangazia Mahusiano ya Kimaana katika Majina ya mahala

Watafiti mbalimbali ambao wametafiti kuhusu mahusiano ya maana ya majina ya mahala miongoni mwao ni pamoja na:

Cameroon (1961) alitafitimajina ya mahali katikajamii ya Waingereza. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa kuna majina yanayohusiana na makaazi pamoja na yale yanayohusiana na sura ama muonekano wa eneo. Akitolea mfano wa majina hayo ni kama vile: "*Stanford Bridge*" yaani sehemu yenye daraja, na "*Greenhill*" akimaanisha eneo lenye kilima chenye kijani kwa wingi. Hata hivyo, Hymes (1964) anaungama na Cameroon (ameshatajwa) kwa  kulithibitisha hilo katika kazi yake iliyozungumzia mahusiano ya lugha, utamaduni na jamii, kwakutueleza kuwa utoaji wa majina ya mahali maranyingi huwa yanatolewa kwa kuakisiwa na fikra za watu pamoja na vipengele vya utamaduni wao. Naye Majepela (2009) alifanya utafiti unaohusiana na majina ya mahali yanavyounda majina ya watu. Katika utafiti wake huo, alibainisha namna majina ya mahali yanavyonyambulishwa kuunda majina ya

watu waishio katika eneo husika pamoja na kubainishaviambishi ngeli vinavyojitokeza katika majina ya mahali.

Pia, Bubwera (2010) alifanya utafiti unaohusiana na majina ya Wahaya, na kubaini kwamba majina ya Wahaya yana uhusiano mkubwa na majina ya mahali. Hivyo anakubaliana na Schotsman (2003) ya kwamba majina hutolewa kwa shughuli wanazofanya watu, sababu za kihistoria, matukio, miti, mimea, wanyama, tabia, utamaduni, majanga ya asili, kama vile: "*Bwero*" yaani mahali palipotumika kunyongea wahalifu.

Hata hivyo, Zubeir (2015) alifanya utafiti unaohusiana na majina ya mahali na mfungamano wa jamii na utamaduni. Katika utafiti wake, aligundua kuwa majina ya mahali yana mfungamano wa karibu sana na jamii husikapamoja na utamaduni wa jamii husika. Pia, Zubeir (ambaye ameshatajwa) anaendelea kutueleza kuwa majina hutokana na hali ya kimazingira kulingana na maeneo husika ya kijiografia yanayoambatana nayo, pamoja na hayo, anadai kuwa kuna baadhi ya majina ya mahali hutokana na watu maarufu au matendo ya kihistoria yaliyofanywa na wakaazi wa zamani wa maeneo husika.

Hivyo basi, kazi za wataalamu wote hao, zimemsaidiana kumuongoza vyema mtafiti katika kulifikia lengo lake la pili la tafiti yetu hii, ambalo liliangazia Kubainisha mahusiano ya maana ya majina ya mitaa na majina ya wadudu, wanyama na ndege.Kwavile kazi hizi zilihusu mahusiano yakimaana baina yamajina ya mahala. Kwa mintarafu hiyo kazi hizi zilimpa mwanga wa kutosha mtafiti katika kubaini

mahusiano, historia na utamaduni baina ya maana ya majina ya wanyama, ndege na wadudu namna yanavyoakisiwa na maana ya majina yamitaa.

#### 2.3.2.2 Tafiti Tangulizi zilizoangazia Mahusiano ya Kimaana katika Majina ya Mitaa

Watafiti mbalimbali walitafiti kuhusu mahusiano ya maana ya majina ya mitaa miongoni mwao ni kama:

Abuubakar (1998) alitafiti kuhusu utoaji wa majina ya mitaa.Katika tafiti yake hiyo alijishughulisha na utoaji wa majina ya Mtoni na Chuini na alibaini kuwa jina la mtaa wa "*Mtoni*" limepewa jina hilo kutokana na jengo kongwe la Sultani wa Zanzibar lililopo pembezoni mwa mto mdogo uliotoka upande wa ndani wa Kisiwa cha Unguja nakupitisha maji yake masafa mafupi baada ya kulipita jumba hilo kuelekea pwani. Pia Abuubakar (ameshatajwa) anatueleza kuwa jina la "*Chuini*" lilibuniwa kutokana na kuwa kulikuwa na jumba kubwa lenye bustani kubwana yenye kuvutia ndani yake ambamo mlikuwa mkifugwa wanyama kama: Chui, Simba na wengine hivyo uendeshaji wa haraki hizo ulichangia kuzuka kwa jina hilo katika mtaa huo.

BAKIZA (2008) linaeleza kwa kutaja majina mengi ya mitaa inayopatikana mjini Unguja, sababu zinazochangia kupewa jina la mtaa husika pamoja na sehemu alizokuwa akiishi mwanasanaa mashuhuri Bwana Msa. Majina ya mitaa ambayo imetajwa na BAKIZA ni pamoja na mtaa wa Kundemba, mtaa ambao ni maarufu kwa upatikanaji wa kinywaji cha aina ya pombe ya kienyeji(Gongo), ngoma ya mbwa kachoka (beni) pamoja na sherehe za tafrija. Vile vile mtaa wa Baraste

kipande, ambao ulikuwa ni mtaa wa kukutanisha tamaduni za majumba ya mawe na ng'ombe.

Masoud (2014) alitafiti kuhusu mchango wa majina ya Vijiji vya Donge katika kuhifadhi historia ya Unguja. Katika tafiti yake hiyo ameonekana kuwa sawa na tafiti ya Abuubakar (ameshatajwa). Kwa kiasi fulani kazizote hizi nimuhimu na zimemsaidia sana mtafiti katika kumpata maarifa ya kihistoria ya majina ya mahala na namna yanavyoakisi uhifadhi wa historia ya Unguja.

Schotsman (2003) alitafiti kuhusu majina ya vituo vya dala dala na mitaa ya Dar es Salaam. Katika utafiti wake huo, alitumia majina ya vituo vya daladala pamoja na majina ya mitaa na kufanikiwa kupata maana ya majina hayo pamoja na kupata historia yake.Schotman (ameshatajwa) katika tafiti yake hiyo akiendelea kutuelezea, kwamba majina yanatokana na majengo kama shule, hospitali, watu maarufu, misikiti, makanisa au hata shughuli zinazofanywa na watu katika eneo hilo. Akitoa mfano: "*Kawawa*", kituo hiki kipo njia panda inayoelekea uwanja wa ndege katika mtaa wa Gongolamboto. Mfano wa majina ya mitaa yanayotokana na mimea iliyopo katika sehemu hiyo, lugha za asili mfano: "*Mwananyamala*" yaani mtoto usilie, asili ya neno hilo ni Kizaramo linalotokana na wanawake walioishi awali katika eneo hilo kutumia usemi huu wakati wakibembeleza watoto wanapokuwa katika shughuli zao za shambani. Majina mengine hutolewa kutokana na maneno ambayo yanashabihiana mfano: "*Mawenzi*" yaani mteremko kama mteremko.

Kwa ujumla, tafiti zote hizi zimemsaidia na kumuongoza vyema mtafiti katika kulifikia lengo la pili la tafiti yetu hii kwa vile zilimpatia mbinu pamoja na njia

muafaka katika kubainisha mahusiano ya maana ya majina ya wanyama, ndege na wadudu yanavyoakisiwa na utoaji wa maana wa majina ya mitaa.

### 2.3.3 Kazi Tangulizi za Kitafiti zilizozungumzia sababu zinazochangia katika Utoaji wa Majina ya Mahala na Mitaa

Watafiti tofauti ulimwenguni walitafiti sababu mbalimbali zinazochangia utoaji wa majina ya mahala na mitaa katika tafiti zao, miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na hawa katika 2.3.3.1 pamoja na 2.3.3.2 hapa chini:

#### 2.3.3.1 Kazi tangulizi za kitafiti zilizozungumzia Sababu zinazochangia katika Utoaji wa Majina ya Mahala

Watafiti tofauti wamezungumzia kuhusiana na utoaji wa majina ya mitaa kwa kuangazia sababu zinazochangia utoajia wa majina hayo miongoni mwao ni pamoja na:

Njozi (2010) katikatafiti yake iliyokuwa imehusiana na mauwaji katika eneo la mwembe kinyongakipindi cha uingiaji wa ukoloni, katika tafiti yake hiyo alifanikiwa kubaini kwamba wakati wa vita vya Abushiri na Wajerumani huko Kilwa, wazalendo walipigana kufa na kupona na Wajerumani kutokana na udhaifu wa wazalendo hao Wajerumani walifanikiwa kuwanyonga wazalendo katika Mwembe, akiwemo Al-ustadh Omar ambaye ni kiongozi wa Waafrika, hivyo kutokana na tukio hilo la kihistoria, ndio maana sehemu hiyo ikapewa nakubambikwa jina la Mwembe Kinyonga.

Naye Mzee (2014) alitafiti kuhusu nafasi ya majina na pepo za Makunduchi katika kuhifadhi utamaduni wa Makunduchi. Akilenga kuchunguza nafasi ya majina katika kuhifadhi utamaduni wa Makunduchi. Katika utafiti huo, amebaini sababu mbalimbali zinazopelekea kupewa majina ya mizimu ya Makumduchi kama: "*Mzimu wa Majipepo* yaani maji baridi yaliyopo kwenye mzimu.

Kwa ujumla, tafiti hizi za Njozi na Mzee ( wameshatajwa), zimemsaidia na kumuongoza vyema mtafiti katika kuchunguza sababu zinazochangia katika utoaji wa majina kupitiavipengele vya kihistoria na kiutamaduni vinavyoakisiwa na utoaji pamoja na upangaji wa majina ya mitaa kupitia majina ya wanyama, ndege na wadudu kama ambavyo tatizo la utafiti linavyo dai.

#### 2.3.3.2 Kazi tangulizi za kitafiti zilizozungumzia sababu zinazochangia katika Utoaji wa Majina ya Mitaa au Vijiji

Watafiti tofauti wamezungumzia kuhusiana na utoaji wa majina ya mitaa kwa kuangazia sababu zinazochangia utoajia wa majina hayo miongoni mwao ni pamoja na:

Chum (1982) alitafiti asili ya mitaa Mkoa wa Kusini Unguja. Akielezea mitaa hiyo, kuwa inatokana na asili ya wanyama. Akisisitiza hili Chum (keshatajwa) anatoa mfano: "*Paje*", kwamba asili yake ni mnyama aitwae Paa, historia ya kilimo cha choroko. Wageni waliofika katika eneohilo walikuwa ni ndugu saba ambao walishauriana kuishi pembezoni mwa pwani ya Unguja ili waendeleze kilimo hiki. Wakati wakijadiliana katikamjadala huo mmoja wao aliuliza kwa kutakakujua kuhusu usalama wa kilimo chao hicho na athari za mnyamaa pamaa kwa kusema

tunalima kilimo cha choroko paa jee? Wakati wakijadili kuhusu uharibifu juu ya mnyama huyu ndipo lilipoibuka jina la mtaa huu kutokana na jina la mnyama na kibainishi cha ulizi yaani “*paa*” - “*je*” sababu hizo ndizo zilizochangia mtaa / kijiji hicho kikaitwa “*Paje*” . Utafiti huu umemsukuma mtafiti kupata pengo la kitaaluma la kutaka kuchunguza sababuzinazochangia majina ya wanyama, ndege na wadudu yanavyoakisiwa na majina ya mitaa.

Naye, Salim (1984) alifanya utafiti kuhusu asili ya vijijivya Kusini Pemba. Akilenga kuchunguzaasili ya vijiji hivyo. Matokeo ya utafiti wake huo yalibainisha kuwa uitaji wa majina ya vijiji ni kutokana na historia. Akitoa mfano: “*Ziwani*”. Akifafanua kuhusuasili ya kijiji hiki anaeeleza kuwa mwanzo palikuwa hapaitwi kwa jina hilo, bali paliitwa “*Mivuno ishirini*”, kwa vile palikuwa na mivuno ishirini na baadae pakaitwa Ziwani kutokana na sababu ya kuwepo ziwa kubwa la maji baridi hivyo jina hilo linatokana na ziwa hilo. Salim (ameshatajwa) akiendlea kutueleza kwa kusema kuwa kila jina la kijiji cha kusini Pemba kinatokana na asili yake kulingana na watu wanaoishi hapo.

Masoud (2005) alitafiti kuhusu asili ya majina ya vijiji na wakaazi wake. Katika utafiti wake huo, alieleza kuwa asili ya jina la kiji cha Mtende linatokana na watu wa Makunduchi ambao walienda kutembea kijiji cha jirani na kuwakuta wenyeji wa huko wakiwa wamelima mazao mengi, na hapo ndipo wageni hao waliposema kuwaambia wenyeji wao ‘*amanyiemtemde*’ wakimaanisha wamefanya kazi kubwa ya kilimo na hapo ndipo wenyeji wao wakajibu “*kwani nyiemjikalii Makunduchi*?” na hii ndio sababu ya kuitwa jina la Mtende. Ufafanuzi huu wa kimaelezo unatuonesha kuwa utafiti wa Masoud (keshatajwa) ulizingatia sababu za asili ya vijiji na wakaazi

wa vijiji husika, hata hivyo utafiti huu hakuchunguza jinsi majina hayo yanavyoakisiwa na sababu zinazotokana na majina ya wanyama, ndege na wadudu katika uteuzi wa majina ya mitaa. Kwa ujumla tafiti hizi za Salim naMasuod (wameshatajwa) zimemsaidia sana mtafiti katika kulifikia lengo la tatu la tafiti yetu hii, pamoja na kumuongoza vyema katika kuchunguza sababu zinazochangia majina ya wanyama, ndege na wadudu kuakisiwa na utoaji wa majina ya mitaa.

Naye Ingram (2007) alitafti kuhusu asili ya neno Zanzibar, katika utafiti wake huo alibaini kuwa asili ya neno Zanzibar ni *"Zinjiba*" ambalo linatokana na lugha ya Kifaransa lenye maana ya ardhi nzuri ya watu weusi. Sambamba na hayo anadai kuwa neno Unguja lina asili ya Kiswahili ambalo linatokana na "*Ungu-jaa*" yaani Kisiwa chenye watu weusi, vyakula tele na ibada nyingi. Kwa upande wa Kisiwa cha Pemba anaeleza kuwa kimetokana na neno la Kiswahili "*kupemba*" lenye maana ya kupembua na kuongoza chombo kwa uangalifu kutokana na kisiwa hiki kuwa kimezungukwa na mkondo mkubwa wa bahari. Kazi hii pia ilikuwa muhimu sana kwa mtafiti kwani imemsaidia kugundua asili ya baadhi ya majina ya mitaa na sababu za uteuzi wa majina hayo.

Ingawaje, taafiti za wataalamu hao, wote zilijikita zaidi kueleza asili za mitaa na maana zake lakini kwa kiasi fulani kazi hizo hazikuzingatia majina hayo ya mitaa jinsi yanavyoakisiwa na majina ya wanyama, ndege na wadudu. Hivyo basi mtafiti ameona kuwa ipo haja ya kuliziba pengo hilo la kutafiti majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa ambalo halikupata kuangaziwa hata kidogo na watafiti mbali mbali waliotangulia.

## 2. 4 Pengo la Kiutafiti

Kutokana na tafiti nyingi alizozipitia mtafiti, aliweza kugundua kuwa wataalamu wengi wao walichunguza maana za majina tofauti kwa kuzingatia vigezo vya kiutamaduni, kimila, kihistoria na kimazingira. Hata hivyo tafiti zote hizo zilijikita katika utoaji wa majina ya sehemu au mitaa kwa kuangalia zaidi asiliya sehemu pamoja namaana tu ya majina hayo na kuacha kuangazia kipengele muhimu cha majina ya viumbe kama vile ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na utoaji wa majina ya mitaa. Hivyo basi mtafiti ameona kuwa kuna haja ya kufanyiwa utafiti hasa katika kuangazia hasa katika kipengele cha majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na utoaji pamoja na upangaji wa majina ya mitaa. Hivyo utafiti huu ulilenga kuliziba pengo hilo kwa kuchunguza kiundani namna majina ya wanyama, ndege na wadudu yanavyowezakuakisiwa na utoaji wa majina ya mitaa, ambapo mtafiti aliamini kuwa hakuna mtafiti hata mmoja aliewahi kuangazia katika kipengele hicho, katika kuliziba ombwe hilo la kiutafiti mtafiti ameongozwa na nadharia ya Semiotiki pamoja na nadhariaJumuishi zikiwemo na mbinu za hojaji, mahojiano, ushuhudiaji pamoja na maktaba.

## 2.5 Kiunzi cha Nadharia

Ili mtafiti aweze kufanikiwa kufanya utafiti wake ni vyema awe na nadharia ambayo itamuongoza ili aweze kujua kuwa atatakiwa kufanya nini, apite wapi na kwa kufuata kigezo gani katika kufanikisha kazi yake ya utafiti. Wataalamu mbalimbali wameleza kuhusu dhana ya nadharia kuwa ni kama fikra au muongozo wa kutekeleza jambo, kutambulika kama ni dhana. Miongoni mwa wataalamu hao: BAKIZA (2000), Verschuren (2005), Sengo (2009). Mdee na wenzake (2011).

Hivyo basi kwaujumla nadharia ni muongozo ambao huelekeza ufanyaji wa jambo katika njia za uhalali, katika kulichunguza na kulitathmini jambo husika.Kwa minajili hiyo nadharia ipo zaidi katika kutoa hoja kulingana na kitu au jambo litakaloshughulikiwa.

Kwa vile majina hutegemea ishara (kiashiria) na kiashiriwa katika jamii, hivyo nadharia ya Semeotiki na Isimu Jumuishi ni nadharia faafu ambazo zimemuongoza mtafiti nakutumikakikamilifu katika utafiti husika.

### 2.5.1 Nadharia ya Semiotiki

Semeotiki ni nadharia inayohusiana na mfumo wa ishara. Nadharia hii inajumuisha uchunguzi, uelewa na utabiri wa maana za ishara na namna zinavyopatikana katika vitu halisi. Kwa ujumla semeotiki ni nadharia inayojishughulisha na utoaji wa fasili za maana zinazolenga ishara mbali mbali katika lugha.

Nadharia hii ya kiisimu imeasisiwa na mwanazuoni wa kiisimu Ferdinand de Saussure. Hata hivyo Mwanaswizz huyu ni miongoni mwa wanafalsafa wa Kipragmatiki kutoka Marekani Peirce.

Hata hivyo Wamitilia (2002:178:179), anadai kuwa msingi mkuu wa nadharia hii kwa mujibu wa muasisi wa nadharia hii ambaye ni De Saussure ni kufafanua lugha kama mfumo wa ishara, ambazo huangaza na kuunda mkufu wa ishara hizo katika lugha. Hivyo kwa De Saussure kila ishara huwa na sehemu mbili, yaani kiashiria (sauti au wasilisho la kimaandishi) na kiashiriwa (maana ya kiashiria). Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kiashiria ni neno lenyewe, na kiashiriwa ni maana

inayopatikana kutokana na kiashiria mfano: ''*mbuzi*'' tutaona kuwa neno mbuzi ni kiashiria na mnyama mbuzi au kifaa cha kukunia nazi ndio kiashiriwa chenyewe.

Vile vile, De Saussure anaelezea kuwa kiashiria ni picha au sauti,wakati ambapo kiashiriwa ni dhana iliyokusudiwa. Naye Brown (1995) anasisitiza kuwa ishara hupata maana kutokana na matumizi yake. Hivyo watu wa jamii moja, wenye kuzungumza lugha moja na kushiriki utamaduni ulio sawa, huwa na makubaliano kuhusu ishara fulani na maana zake. Ishara hizo hujumuisha picha, rangi, maumbo mbalimbali na hata herufi zinazounda maneno.

Sambamba na hayo Griffen (1997:57-58) katika kuelezea maana ya maana, anadai kuwa ishara ni kama kitu tunachokumbana nacho moja kwa moja na huweza kuashiria kitu kingine tofauti. Akiendelea kusisitiza ni kwamba majina au maneno huchukuliwa kuwa ni ishara, kwa sababu hupewa maana na watu. Wamitilia pamoja na Griffen (wameshatajwa) wanaungama pamoja kuwa ishara hutumiwa kueleza kitu fulani.Wakiendelea kufafanua zaidi wanaeleza kuwa ishara huwakilisha kitu kingine katika uhusiano uliopo kati ya vitu hivyo viwili au ni uwezo wa kuibua fikra fulani katika akili ya msomaji.

Kwa minajili hiyo, nadharia ya Semiotiki inazungumzia ishara ambazo zinaeleweka na mjunzi wa lugha husika.

Sambamba na hayo nadharia ya Semiotiki iliwahi kutumiwa na watafiti mbali mbali katika suala zima la kiutafiti wa ishara na maana zake. Miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na Wacharo (2013) aliitumia nadharia hii katika tafiti yake iliyoangazia

"*Kanga kama sajili maalum ya kisanii na mawasiliano".* Ambapo nadharia hii ilimuwezesha kufasiri maana za majina na jinsi yanavyopatikana katika vazi la Kanga na kuweza kutoa matokeo kuwa majina ya kanga ni kweli sajili maalum katika mawasiliano. Hata hivyo James (2010) aliitumia nadharia hii katika kutafiti "*Maana zamajina ya watu wa kabila la Lulugoodi".* Ambapo ilimsaidia sana na kupata mafanikio makubwa katika kutoa maana za majina ya watu wa kabila hilo.

Pamoja na hayo Kilanga (2014) naye aliitumia nadharia hii katika tafiti yake iliyolenga kuchunguza "*Ishara katika kaptula la Max na kijiba cha moyo"* ilimsaidia na kufanikiwa kutoa ishara za Kimax na Kijiba cha moyo jinsi zinavyojidhihirisha katika uvaaji wa kaptula kwa vijana. Hata hivyo nadharia hii ni faafu katika utafiti huu, kwaniimemsaidia mtafiti katika kulifikia lengo la pili la utafiti huu, kwavile imemuwezesha kubaini na kuchambua mahusiano ya maana ya majina ya mitaa namajina ya wadudu, wanyama na ndege jinsi yanavyotumika katika uteuzi wa majina wa mitaa hiyo. Kwa vile nadharia hii ilijikita katika kuangalia maana ya ishara tu hivyo ilimlazimu mtafiti kutumia nadharia nyengine ili kuweza kukamilisha lengo la kwanza na la tatu la utafiti huu.

### 2.5.2 Nadharia Jumuishi

Nadharia hii imeasisiwa na Giles mnamo mwaka (1979). Msingi mkuu wa nadharia hii, unazingatia fasili ya jamii lugha unaosema, jamii inaundwa na wale watu wanojiona na kujitambua wenyewe Giles (1979:253).

Hivyo nadharia jumuishi hujikita zaidi na maana halisi ya utambulisho. Giles (keshatajwa) akiendelea kufafanua na kuelezea kuwa, utambulisho wa mtu au jamii

ni mchakato unaoendelea ambao unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamii lugha ambayo huunda kiini cha utambulisho wa jamii husika, vibainishi hivyo ni pamoja na majina. Hata hivyo Giles anasisitiza kwamba maana halisi ya utambulisho baina ya jamii lugha moja na nyingine hutokana na mambo yao ya msingi yanayotokana na utamaduni, mila na desturi, imani za kidini, vyakula, mavazi, uchumi na hata katika mambo ya kisiasa. Nadharia hii iliwahi kutumiwa na wataalamu mbalimbali na kuwasaidia katika kufanikisha na kukamilisha malengo ya kazi zao, miongoni mwao ni pamoja na Msanjila (2009) katika kutafiti wake "*Majina ya watu wa kabila la Wachaga"* katika tafiti yake hiyo amefanikiwa kutoa maana za majina mbali mbali yanayojitokeza katika kabila la Wachaga, vile vile ilimsaidia katika kubaini sababu za uteuzi wa majina katika kabila la Wachaga na maana zake.

Naye Zubeir (2015) ameitumia nadharia hii katika utafiti wake *wa "Etimolojia ya majina ya mahali, Kaskazini Pemba kuwa utambulisho wa utamaduni wa Wapemba."* Ilimsaidia katika kufafanua na kubaini vigezo vinavyotumika katika kuakisi majina ya mahali ya Kaskazini Pemba.

Kutokana na mafanikio waliyoyapata watafiti hao, mtafiti ameona ni vyema akatumia nadharia hii katika utafiti wake uliolenga kuchunguza majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisi majina ya mitaa na ilimsaidia kufikia na kufanikisha lengo la kwanza na la tatu la utafiti wake.

## 2.6 Muhutasari wa Sura

Sura hii imeangazia mapitio ya kazi tangulizi mbali mbali, imeonesha mwanya wa utafiti, viunzi vya nadharia vilivyotumika kati ya nadharia ya Semeotiki na Jumuishina kumalizia na muhtasari wa sura. Sura inayofuata ni mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imeonesha mbinu zilizotumika katika kufikia malengo ya utafiti huu. Katika kipengele hiki, mambo muhimu yafuatayo yamefafanuliwa: eneo la utafiti, mkabala wa utafiti, njia za kukusanyia data, sampuli na usamulishaji, vifaa vilivyotumika katika utafiti, uchambuzi wa data na mwisho imeonesha hitimisho la sura.


## 3.2 Eneo la utafiti

Utafiti huu umefanyika katika kisiwa cha Unguja. Kisiwa hiki kinajumla ya Mikoa mitatu yenye Wilaya Saba. Mkoa wa Kaskazini Unguja una jumla ya Wilaya mbili: Wilaya ya Kaskazini "A" na "B". Kwa upande wa Mkoa wa Kusini Unguja nao unajumla ya Wilaya mbili: Wilaya ya Kusini na ya Kati. Hata hivyo Mkoa wa Mjini Magharibi ambao unajumuisha ya Wilaya tatu ambazo ni Mjini, Magharibi "A" na "B". Kielelezo nambari 3:1 hapo chini kinaonesha maeneo hayo yaliyotajwa.Wilaya zote hizi zimehusika na utafiti huu.

Mtafiti aliamua kuteua maeneo haya kwa sababu ndio sehemu pekee ambayo ina majina mbalimbali ya mitaa inayohusiana na tatizo la utafiti, vilevile mtafiti ni mzaliwa miongoni mwa moja kati ya Wilaya hizo, hivyo ana uwelewa pamoja na uhusiano wa karibu na wakaazi wa maeneo husika, sambamba na hayo mtafiti alikuwa na uhakika wa kuwapata watu mashuhuri, ambao wameweza kumpatia historia halisi ya mazingira na hata tamaduni za mitaa katika maeneo teule ya utafiti. Hivyo kutokana na sababu hizi, mtafiti ameona ni vyema kuyateuwa maeneo hayo kwani amehisi ni maeneo faafu yaliyoweza kumpatia data za uhakika

zilizomuwezesha kuyafikia malengo matatu pamoja na kuyajibu kwa ufasaha kabisa maswali ya utafiti huu.

Kielezo Na. 3:1 Ramani ya Unguja ikionesha mikoa yake mitatu (Kaskazini, Kusini na Mjini Magharibi Unguja)




[http://www.maphill.com/tanzania/kaskazini-unguja/location-maps/political-map/?most-similar-to=maps/political-map/](http://www.maphill.com/tanzania/kaskazini-unguja/location-maps/political-map/?most-similar-to=maps/political-map/) Iliyopakuliwa tarehe 20 Oktoba, 2018

### 3.3 Mkabala wa Utafiti

Mkabala wa utafiti ni muundo wa kidhanifu ambao huuongoza utafiti katika mpangilio au utaratibu wa kukusanya na kuchanganua data katika hali ambayo inalenga kufikia malengo ya utafiti (Kombo na Tromp, 2006). Kwa minajili hiyo sasa Utafiti huu umetumia mkabala wa kimaelezo zaidi katika kuzichakatua na

kuzichambua data za uwandani ambazo zilizokusanywa na mtafiti kupitia watafitiwa wake.

Creswell (2002) anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo ni mkabala wa kielimu ambao mtafiti hutegemea kukusanya data kwa kiasi kikubwa cha maneno au matini na kuzichambua kwa maelezo. Hivyo masuala mbalimbali yaliyohusiana na majina ya wanyama, ndege na wadudu yamefafanuliwa kwa kutumia mkabala huu.

Mtafiti alitumia mkabala huu kwa kuzichambua data alizozikusanya kutoka uwandani kwani data hizo zilihitaji kufafanuliwa kwa mbinu za kimaelezokwa vile data hizo zimehusu simulizi za kale zilizohusu majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoaakisiwa na uteuzi wa majina ya mitaa, pamoja na kuonesha idadi ya watafitiwa kwa kuwaweka katika jedwali ambalo limeonesha idadi halisi ya watafitiwa waliotumika katika utoaji wa taarifa zilizohusu tafiti hii.

## 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti ni kundi la watu, ambao mtafiti amekusudia kuwatumia katika utafiti wake (Kombo na Tromp, 2006). Walengwa wa utafiti huu ni watu wazima wa kike na wakiume ambao ni wakaazi wa maeneo husika kutoka Wilaya saba za mikoa mitatu ya Unguja, walengwa hao ni wazaliwa halisi katika maeneo yaliyofanyika utafiti huu.

### 3.4.1 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni kitu au vitu kati ya vitu vingi vya aina moja ile ile vinavyochukuliwa kama mfano mzuri wa vitu hivyo TUKI (2004).

Hivyo, Sampuli ni watu, vitu au maeneo ambayo aliyoyateuwa mtafiti kwa niaba ya walengwa wa utafiti katika kuhakikisha kufanyika uchunguzi baina yao kwa sharti la kupata taarifa stahiki juu ya mada husika. Hivyo basi, katika utafiti huu jumla ya watoa taarifa 70 walitumika katika kupata data zilizohusiana na malengo pamoja na maswali ya utafiti huu. Watoa taarifa hao walikuwa katika mgawanyo maalumu kama ufuatao:

**Jedwali na. 3.1: Linaonesha sampuli ya Watoa Taarifa**

| WILAYA | WATOA TAARIFA | | |
|---|---|---|---|
| | W / KE | W/ME | JUMLA |
| Kaskazini A | 5 | 5 | 10 |
| Kaskazini B | 5 | 5 | 10 |
| Kusini | 5 | 5 | 10 |
| Kati | 5 | 5 | 10 |
| Mjini | 5 | 5 | 10 |
| Magharibi A | 5 | 5 | 10 |
| Magharibi B | 5 | 5 | 10 |
| | JUMLA YA WATOA TAARIFA 70 | | |

Katika kila wilaya watafitiwa 10 walitumika katika kutoa taarifa wakiwemo wanawake watano na wanaume watano. Katika kupata sampuli hiyo, mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji lengwa,kwa kuwateua watu maalumu wenye umri usiopungua miaka hamsini (50) na kuendelea kwa lengo la kumpatia data za uhakika kwa vile mtafiti aliamini kuwa sampuli ya namna hiyo imeishi maeneo husika kwa

muda mrefu na hivyo itakuwa inaelewa historia ya majina ya mitaa yao kwa kina na kuwezeshaukamilishaji wa utafiti huu.

### 3.4.2 Usampulishaji Lengwa

Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kuwa mbinu hii ya usampulishaji, mtafiti kwa makusudi huchagua watu ambao anaamini wana taarifa za kutosha na faafu kuhusu utafiti wake. Mtafiti alitumia sampuli hii, kwa madhumuni ya kupata tarifa za uhakika kutoka kwa watafitiwa wake katika mitaa ama vijiji husika. Kwa hiyo, mtafiti alikusanya taarifa kutoka kwa watafitiwa 70, na alikwenda moja kwa moja kwa walengwa na kuwaomba taarifa zilizomsaidia katika kufikia malengo ya utafiti huu.Vile vile mtafiti ameiteua mbinu hii kwa sababu ilimuwezesha kupata watoa taarifa wenye uweledi ambao kwa kiasi fulani waliweza kumpa data halisi zilizotumika katika utafiti huu.

## 3.5 Aina za Data

Katika utafiti huu mtafiti alitumia data za aina mbili, data za maktabani na data za uwandani kwa lengo la kufanikisha malengo matatu ya utafiti huu ambayo ni kubainisha majina ya wanyama, ndege na waduduyanavyotumika kuwakilisha majina ya mitaa, kuainisha mahusiano ya maanaya majina ya mitaa na majina ya wadudu, wanyama na ndege na mwisho kuchambua sababu zinazochangia majina ya mitaa kuakisiwa na majina ya wanyama, nadege na wadudu.

### 3.5.1 Data za Maktabani

Kwa vile utafiti huu umehusika na majina ya wanyama, ndege na wadudu, data za maktabani zimetumika kwa kiasi fulani kwa sababu muelekeo wa mada husika

umejikita zaidi mambo ya kihistoria ambayo maranyingi huwa yameandikwa na wataalamu mbalimbali. Hivyo, mtafiti alidurusu majarida,vitabu mbalimbali vilivyoandika kuhusu majina ya wanyama, ndege na wadudu, kazi ambazo zilimuwezesha mtafiti kuona majina hayo yalivyooana na tatizo pamoja na malengo matatu ya utafiti huu kwa ajili ya kupata na kutanua wigo wa kitaaluma. Katika kuzifatilia data za namna hii, mtafiti alilazimika kutembelea maktaba za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Maktaba Kuu ya Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA). Zilitumika maktaba hizi kwa sababu ndimo mnamopatikana machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafi na zilimsaidia katika kupata taarifa muhimu ambazo zilimsaidia kuyafikia malengo yake ya utafiti.

### 3.5.2 Data za Uwandani

Katika kukusanya data za uwandani mtafiti ametumia mbinu ya hojaji, mahojiano na ushuhudiaji, ambapo mbinu hizi zimeteuliwa kwa kuwa zilifaa zaidi katika kukusanya data zilizohitajika katikakuyakamilisha malengo ya utafiti huu.

## 3.6 Mbinu za Kukusanyia Data

Kothar (1990) anaeleza kuwa mbinu za kukusanya data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Best na Kahan (1993) wanalithibitisha hili kwa kueleza kuwa katika ukusanyaji wa data ni muhimu kutumia mbinu zaidi ya moja kwani kila mbinu ya ukusanyaji data ina ubora na changamoto zake. Hivyo, utumiaji wa mbinu zaidi ya moja husababisha mbinu moja wapo kupunguza changamoto za mbinu nyingine na kuongeza ubora wa utafiti. Hivyo Utafiti huu umetumia mbinu za hojaji, mahojiano ya moja kwa moja na watafitiwa sambamba na kushuhudia

maelezo sahihi yanayohusiana na mitaa pamoja na vijiji kutoka uwandani ili kukidhi haja ya malengo husika.

### 3.6.1 Mbinu ya Hojaji

Neuman (1991) anaeleza kuwa hojaji ni mbinu ambayo mtafiti anaweza kupata watafitiwa wengi kwa muda mfupi. Akilithibitisha hili (Cohen, 2001) kwa kueleza kuwa mbinu hii humuwezesha mtafiti kupata data nyingi na kufanya majumuisho ya matukio, mawazo na kuelezea uhalisia uliopo. BAKIZA (2010) linaeleza kuwa hojaji ni karatasi yenye maswali ya utafiti kuhusu jambo maalumu kiudadisi. Mtafiti alichagua mbinu ya hojaji na kukusanya data ambazo zilizohusiana na majina yamitaa ambayo yanaakisiwa na majina ya wanyama,ndege na waduduambapo data hizo alizipata kutoka kwa watoa taarifa wengi kwa muda mfupi. Ingawaje mtafiti alipata majibu kwa muda mfupi lakini pia alilazimika kutumia mbinu ya mahojiano na ushuhudiaji kwa vile wengi wa watafitiwa wake ni watu wazima ambao hawana uwelewa mzuri katika kusoma na kuandika hivyo ilimlazimu kutumia mbinu nyingine ili kuyafikia malengo ya tafiti hii.

### 3.6.2 Mbinu ya Mahojiano

Kwa mujibu wa Mulokozi (1983) mahojiano ni maelezo ya ana kwa ana au simu, kidijitali (barua pepe) kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa. Halikadhalika, mbinu hii inaelezwa na Enon (1998) kuwa mtafiti anaweza kukusanya taarifa inayohusisha uulizaji wa maswali kwa njia ya ana kwa ana. Mtafiti hivyo wanyama, ndege na wadudu na kuweza kugundua jinsi majina hayo yanavyoakisiwa katika utoaji wa majina ya mitaa. Ambapomtafiti alipata fursa kuwauliza watoa taarifa maswali ya

ziada na kupata majibu papo hapo na hata kwa yale masuali yaliyokosa ufafanuzi katika mbinu ya hojaji yalipatiwa ufumbuzi. Sambamba na hayo mtafiti alishawishika kutumia mbinu ya ushuhudiaji ili kuweza kushuhudia maongezi yanayohusiana na historia, mila, tamaduni na hata harakati za kiuchumi na kijamii zilizohusiana na mitaa husika.

### 3.6.3 Mbinu ya Ushuhudiaji

Mtafiti alilazimika kufika katika mitaa ya watoa taarifa na kushuhudia maongezi waliyoongea kuhusu majina ya mitaa ambayo yalimuwezesha kujua ukweli kuhusiana na mitaa husika, na aliweza kugundua mahusiano ya maana ya majina ya mitaa, sababu zinazochangia na kuwakilisha majina ya viumbe kama wanyama, wadudu na ndege jinsi yanavyoakisiwa na utoaji wa majina ya mitaa. Hata hivyo mtafiti ilimlazimu kutumia vifaa vya kunasia sauti kama vile simu za mkononi kwa lengo la kurikodi sauti za watafitiwa wake ili kupata data za uhakika kutoka kwao, ambazo zilimuwezesha mtafiti kuyafikia malengo yake ya utafiti huu.

## 3.7 Vifaa vya Utafiti

Ili kufanikisha utafiti huu vifaa mbalimbali vilitumika katika kukusanya na kuhifadhia taarifa. Vifaa hivyo: daftari, kalamu, kumputa-mpakato, simu ya kiganjani, kinyonyi na sidii. Daftari na kalamu vilitumika kunukuu taarifa mbalimbali zilizokusanywa kutoka kwa watoa taarifa na maktabani pamoja na kuhifadhia taarifa mbalimbali: tarehe, siku, muda mahali na umri wa watoa taarifa. Komputa-mpakato ilitumika kuhifadhi data, na kufanyia uchambuzi wa data na maandiko pamoja na pendekezo la utafiti huu. Simu ya kiganjani ilitumika kuwasiliana na watoa taarifa pamoja na kurikodia sauti na mazungumzo ya watoa

taarifa. Kinyonyi na sidii vilisaidia kuhifadhia data pamoja na pendekezo la utafiti.

### 3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Katika kuchambua data za utafiti huu, mbinu ya uhakiki ilitumika katika utafiti huu. Hivyo mtafiti alipanga majina hayo na kuyanakili kwa kuyabagua katika makundi yanayohusika kisha kuzichambua data, sambamba na hayo mtafiti alizichambua taarifa za watafitiwa wake kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Mkabala huu ulitumika katika kuyapanga majina katika kila kundi kutokana na aina ya majina hayo. Vile vile mkabala huu ulitumika kwa sababu ya kuona historia ya majina yalivyotolewa na watoa taarifa hao, kwa vile majina hayo yalitokana na majina ya wanyama, ndege, na wadudu jinsi yalivyoakisiwa na utoaji wa majina ya mitaa kwa mujibu wa wakaazi na watoa taarifa wa mitaa husika.

### 3.9 Uwasilishaji na Uchambuzi wa data

Uwasilishaji naUchambuzi wa data ni sehemu muhimu katika kukamilisha utafiti uliolengwa kufanywa namtafiti kwa namna moja au nyingine. Kothari (2008) anaeleza uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika utafiti ambayo husaidia kutafuta majibu ya tatizo la utafiti. Hivyo kuna mikabala miwili mikuu ambayo hutumika sana katika uchambuzi wa data za kiutafiti ambayo ni uchambuzi wa kimaelezo pamoja na uchambuzi wa kitakwimu. Enon (1998) anaelezea kuwa mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data ambapo mtafiti hueleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo. Sambamba na hayo mtafiti alitumia uwasilishaji na uchambuzi wa kimaelezo,michoro ya ramani pamoja na majedwali yote haya aliyoyafanya ni kutokana na kuwa tatizo la utafiti huu lilihusiana na maelezo zaidi kuliko kimahesabu katika kuitumia mbinu hiyo wakati

wa kuchambua data, ameambatanisha na michoro ya majedwali. Hivyo uwasilishaji huu wa kimaelezo ni muhimu sana kwa mtafiti kwani ulimuongoza vyema na kwa urahisi katika kuzichambua data zilizotokana na maswali ya utafiti huu pamoja na kufikia lengo kuu la utafiti pamoja na malengo mahsusi ambayo mtafiti alidhamiria kwadhati kabisa kuyafanyia kazi na kuyapatia ufumbuzi wa kina.

## 3.10 Muhutasari wa Sura

Kwa ujumla sura hii imeeleza mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Mbinu hizo zimeelezwa na kufafanuliwa namna zilivyotumika. Mbinu hizo ni eneo la utafiti, mkabala wa utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na usampulishaji, aina za data, mbinu za ukusanyaji wa data, vifaa vya utafiti, mbinu za uchambuzi wa data na kumalizia na uwasilishaji na uchambuzi wa data na muhutasari wa sura.Sura inayofuata ni uchambuzi wa data uwasilishaji wa matokeo na majadiliano.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuzichambua data pamoja na matokeo ya utafiti sambamba na majadiliano yaliyojitokeza katika utafiti huu.

**Maana ya matokeo ya utafiti**

Matokeo ya utafiti ni zile data, habari, taratibu, mbinu, matokeo, njia, teknolojia na maelezo ya utafili huu. Matokeo ya utafiti hutumika kuelezea habari zote za nyuma zinazohusiana na utafiti (Creswell, J.W (2008).

**Maana ya majadiliano**

Wataalamu mbalimbali wamelitolea maana neno majadiliano kwa kusema:
Hyman (1980) anasema kwamba majadiliano yanachangia kupata suluhisho au jibu la matatizo kulingana na hali au mazingira ya jamii husika.

Nao Gage na Berliner (1988) wanasema kwamba majadiliano ni mahali ambapo wanafunzi wanakusanyika kuelezeana wenyewe kwa umakini na kwa usahihi, kusikiliza mawazo tofauti ya wanafunzi ambao wanaeleza kitu kile kile kwa mitazamo tofauti hatimaye na kupata mwafaka.

Katika majadiliano hupatikana makundi mawili ambayo moja husimama upande wa kuongoza majadiliano hayo na kundi jengine huwa linatoa ushauri au hata kutoa mawazo mapya juu ya kile kinachojadiliwa. Ambapo hii haina tofauti kati yamwalimu na wanafunzi wake wakati wa kuwasilisha mada kwani mwalimu huwa

kiongozi na wanafunzi huwa ndio washiriki na mwisho wa majadiliano hupatiwa suluhisho linalofaa kulingana na mada husika.

Katika sura hiimtafiti amechambua data zilizopatikana uwandani na maktabani.Uchambuzi ambao umefanyika kwa kutumia viunzi viwili vya nadharia kati ya semiotiki na nadharia jumuishi katika kuyakamilisha malengo ya utafiti.Sambamba na hayo sura hii iliwasilisha matokeo na kuyajadili kwa mujibu wa hoja mbalimbali za wataalamu kama ilivyo kwenye mapitio ya kazi tangulizi katika tasnifu hii.

Uchambuzi wa data katika sura hii umehusisha malengo mahsusi ya utafiti huu pamoja na kuyajibu maswali ya utafiti. Baada ya kuzikusanya na kuzipanga data zilizopatikana, hatua inayofuata ni ya kujadili matokeo ya utafiti katika kila kipengele kwa kuhusisha majina ya mitaa husika.

## 4.2 Majina ya Wanyama ndege na Wadudu Yanavyowakilisha Majina ya Mitaa

Mtafitialikusanya taarifa za majina ya mitaa ambayo inahusika katikautafiti wake na mbinu ya hojaji, ushuhudiaji pamoja na mahojiano zilihusika, ambazo zilimuwezesha mtafiti kupata taarifa ambazo zinaonesha uhalisia wa majina ya mitaa kuwa yanatokana na wanyama,ndege na wadudu katika Kisiwa cha Unguja, Mfano wa mitaa hiyo ni Kiziwa Ndege,Kishunga mbuzi, Mwembe Punda, Kiunga Ndege, Kicheche, Mwembe Popo na mengineyo.

Katika utafiti huu mtafiti aliweza kubaini kwamba kila jina la mtaa hutolewa kutokana na vigezo vya kihistoria ama kiitikadi pia majina hayo hutolewa kutokana na athari za kiutamaduni, kijamii, kimazingira na hata kimashuhuri (umaarufu). Kwa vile kila mtaa huwa na asili yake ya uibukaji wa jina la mtaahuo, pamoja na hayo mtafiti ameweza kubaini ya kwamba kila jina lina asili nachanzo chake.

Kama ambavyo Zubeir (2015) katika tafiti yake ya Etimolojiaya Majina ya Mahali ya Kaskazini Pemba kuwa Utambulisho wa Utamaduni wa Wapemba, alibaini kuwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba kuwa kuna majina ya miji yenye asili ya kibantu ama Wareno, pia kuna miji iliyotokana na lengo la kuupanua mji wa Wete yanayotokana na sifa za wakaazi wa sehemu husika, hata hivyo Zubeir (ameshatajwa) anadai kuwa kuna mitaa ambayo ilianzishwa na watu wa mbegu nyeupe kama vile Wahindi na Waarabu na mitaa hiyo kubeba sifa za watu hao. Kutokana na hayo sasa, mtafiti wa utafiti huu alipata fursa ya kupita uwandani kwa ajili ya kupata maelezo ya kina kabisa yanayohusu asili ya vijiji mbalimbali katika mikoa mitatu ipatikanayo kisiwani Unguja. Kwa minajili hiyo kila mtafitiwa alitakiwa aeleze asili ya sehemu anayoishi yeye mwenyewe, na walifanikiwa kutoa maelezo yaliyomsaidia mtafiti kufikia uchambuzi na uchanganuzi anuai ulioakisi malengo matatu ya utafiti huu.

### 4.2.1 Uteuzi wa Jina la mtaa wa Kiziwa Ndege

Kiziwa Ndege ni moja kati ya mitaaya kihistoria inayopatikana Kusini mwa Kisiwa cha Unguja. Mtaa huu unapatikana Mkoa wa Kusini Unguja Wilaya yaKati katika kijiji cha Unguja Ukuu Kaipwani.Kwa upande wa Magharibi mwa mtaa huu umepakana na mikoko pamoja na Kisiwa cha Uzi, Mashariki umepakana na Bonde

kubwa ambalo lasemekana hapo zamani lilikuwa ni ziwa lililokuwa likitumiwa na wakulima kwa kilimo cha umwagiliaji, na hata ndege wa aina tofauti walikuwa wakilitumia ziwa hili kwa ajili ya kuogelea na kunywa maji. Sambamba na hayo mtaa huu ukitokea mjini Unguja una umbali wa meli 20.

Kiziwa ndege ni mtaa ambao yasemekana Wasomanga kutoka mrima ndipo walipokuwa wakiishi.Walifika hapo na kuanza harakati zao za ufugaji pamoja na kilimo cha mpunga, kutokana na harakati hizo ndipo likaibuka jina la Kiziwa Ndege.Kwa vile wakaazi wa eneo hilo walikuwa wakilima mpunga ambao ulikuwa ukiliwa na ndege na baada ya ndege hao kula mpunga huo huelekea upande wa lile bonde na kunywa maji na ndipo wakaazi wa mtaa huo wakaupa jina mtaa huo kuwa ni Kiziwa Ndege. Jina hilo linatokana na majina mawili yaliyofanyiwa miambatanisho ambayo ni Ziwa linalotokana na hilo bonde na Ndege ambao huenda kunywa maji katika Bonde hilo. Nakufanyiwa mchakato wa uwambishaji kwa kuongezewa kiambishi “ki” mwanzoni mwa hilo jina na kupatikana Kiziwa Ndege.

**Ki + mzizi wa neno (Ziwa) + mzizi wa neno (Ndege) ----------------Kiziwa Ndege.**

Kwa ujumla tunaweza kufafanua kuwa kuna uwiano wa hali ya juu kuhusu asili ya jina la mtaa wa Kiziwa ndege na Ndege ambao waliokuwa wakipatikanwa katika eneo hilo, kwani watoa taarifa karibia ya wote waliona kuwa jina hili liliteuliwa na wasomanga waliotokea mrima kutokana na harakati za kijamii na kiuchumi walizokuwa wakizifanya katika sehemu hiyo kwa vile wengi wa watoa taarifa walisema kuwa wakaazi wa awali wa mtaa huo walikuwa ni watu wa kabila la wasomanga ambao walikuwa wakilima mpunga na pembezoni mwa mashamba yao

kulikuwa na bonde kubwa la maji ya kutuwama mithili ya Ziwa, hivyo baada ya mpunga kupea na kuchanua kulikuwa na ndege tofautiwakiwemo Mahuwa,Mnana, Chozi, Msese, Ninga na Pugi.Ndege hao walikuwa wakiula mpunga huo na kisha kwenda kunywa maji katika bonde hilo na hapo ndipo pakaibuliwa jina la Kiziwa Ndege kutokana na mkusanyiko wa maji hayo katika bonde hilo jina ambalo limetokana na kanuni ya Kimofolojia kupitia mchakato wa uambishaji na uambatanishaji.Jina hilo likiwa na lengo la kuwatambulisha watu kuwa eneo hilo ni eneo la mkusanyiko wa ndege tofauti ambao hukata kiu zao kwa maji hayo. Hivyo basi, kutokana na maelezo ya watafitiwa tunaona namna nadharia ya jumuishi ilivyoweza kumsaidia mtafiti katika kubainisha utambulisho wa uteuzi wa mtaa wa Kiziwa ndege kwa kuitambulisha jamii ya mtaa huo na shughuli zao za kiuchumi ambazo zilizokuwa zikifanyika katika eneo husika na kupelekea kuibuka jina la mtaa wa Kiziwandege.

### 4.2.2 Uteuzi wa jina la mtaa wa Kisima Ng'ombe

Kisima Ng'ombe ni miongoni mwa mitaa yenye historia katika upewaji wa jina lake. Kisima Ng'ombe ni mtaa unaopatikana katika Mkoa wa Mjini Magharibi Wilaya ya Mangaribi ‘B’ Unguja ndani ya kijiji cha Bweleo. Mtaa huu umepakana na mtaa wa Bwefumu kwa upande wa kusini naNyamanzi kwa upande wa Kaskazini ama kwa upande wa Mashariki ya mtaa huu kuna bahari hata hivyo kwa upande wa Magharibi mtaa huu umepakana na uwanja wa mpira wa Bweleo.

Wakaazi wa Kisima Ng'ombe ni watu wenye asili ya Wahadimu ambao walihamia hapo kutokea Tanzanania Bara kutokana na taarifa za watafitiwa walisema kuwa wakaazi wa kisima Ng'ombe

wengi wao walikua wakijishuhulisha na harakati za ufugaji wa Ng'ombe ingawaje walikuwa hawana taaluma yoyote ya ufugaji kama vile kuwapatia kinga za kuwalinda na majanga ya maradhi. Hivyo basi mnamo mwaka(1946) Idara ya mifugo iliamua kwa makusudi kuchimba kisima kwa legno la kuanzishwa mradi wa kuwakinga Ng'ombe hao kutokana na maradhi,hasa yakiwemo maradhi ya ndui kwani maradhi hayo ni hatari sana kwa Ng'ombe.

Hivyo, kulilazimika kuchimbwa hodhi moja refu lililokuwa likitiwa maji yatokanayo na kisima hicho na kuchanganywa na dawa na kisha Ng'ombe hao kutumbukizwa humo kwa lengo la kuwakinga Ng'ombe hao na maradhi kupitia maji hayo ya dawa. Pamoja na hayo mradi huo ulianzishwa na mzungu aliyekuwa akitambulika kwa jina la Dicter. Hata hivyo Kisima hicho kilitumika katika utoaji wa huduma hiyo hadi vijiji vya jirani vikiwemo Fumba, Bwefumu, Shakani na hata Kombeni.

Kutokana na harakati za kisima hicho kutambulika na wengi katika utoji wa huduma hizo hapo ndipo lilipopatikana jina la mtaa wa Kisima Ng'ombe na hadi sasa kisima hicho kipo ila hakitumiki tena kwa shughuli za ufugaji bali kinatumika katika shughuli za kawaida ikiwemo majumbani, misikitini nakwengineko.

Jina hili la mtaa wa Kisima Ng'ombe limebuniwa kupitia mchakato wa kimofolojia kupitia kanuni ya uambatishaji maneno, kwa vilejina hili linatokana na nomino mbili ambazo ni “Kisima” pamoja na “Ng'ombe” zilizoshikanishwa pamoja ili kuunda jina moja kutokana na harakati za kuwafikisha Ng'ombe hao kisimani hapo kwa lengo lakutiwa dawa iliyochanganywa na maji ya kisima hicho.Hivyo basi nomino huru hizozimewekwa pamoja na kuunda jina moja la Kisima Ng'ombe kupitia kanuni hii ya muambatano.

**Mzizi wa nomino (kisima) +mzizi wa nomino (Ng'ombe) _____ Kisima Ng'ombe.**

Sambamba na hayo historia halisi inayotokana na jina la Kisima Ng'ombe, watafitiwa wote walisema kuwa jina hilo limetolewa kutokana na kisima kilochochimbwa hapo pamoja na harakati zilizokuwa zikifanyika kwa hao Ng'ombe katika eneo hilo. Ambapo inadhihirisha wazi kuwa nadharia ya semiotiki ilimsaida mtafiti katika kuchunguza maana ya fasili zinazolenga ishara mbalimbali katika lugha na kupelekea maana hizo kusadifu katika uteuzi wa majina yakiwemo ya mitaa kama tulivyoona katika uteuzi wa jina la Kisima Ng’ombe.

### 4.2.3 Uteuzi wa jina la mtaa wa Mwembe Majogoo

Mwembe Majogoo ni mtaa unaopatikana katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, Wilaya ya Kaskazini ‘A’ na unakadiriwa kuwa na umbali wa maili 16 kutoka mjini Unguja katikati ya shehia ya Mbaleni jimbo la Kitope, na umepakana na shehia ya Kitope pamoja na shehia ya Gana.

Asili ya wakaazi wa Mwembe Majogoo ni wahamizi kutoka Tanzania Bara wanaotokana na makabila tofauti wakiwemo Wamwera, Wamakonde, Wandengereko, Wanyamwezi na Wazaramu.

Kwa sasa wakaazi hao wanajishughulisha zaidi na kilimo cha mazao ya chakula na biashara pamoja na usasi wa Nguruwe.

Kwa mujibu wa maelezo na maandishi ya watoa taarifa wameeleza kuwa sababu kuu ya kuteuliwa jina la Mwembe Majogoo kulikuwa kuna Mwembe mkubwa sana ambapo chini ya mwembe huo palikuwa pakipiganishwa majogoo makubwa ya (aina

ya kuchi), ni kama mchezo wao wa kamari na pindi Jogoo la mmoja wapo likishinda basi mshindi huwezakuidhinishiwakulichukua Jogoo lililoshindwa pamoja na pesa ambazo hutolewa na mtu ambaye Jogoo lake limeshindwa katika shindano hilo.

Watu waliokuwa wanajishughulisha na mchezo huo wa Majogoo walikuwa wakitokea sehemu mbalimbali za kisiwa cha Unguja,zikiwemo za Kaskazini kama vile sehemu za Kidoti, Mkokotoni na Kinyasini, hata hivyo wale wanaotokea Kusini walikuwa wakitokea maeneo ya Dunga na kwa wale waliotokea Mkoa wa Mjini Magharibi walitoka katika maeneo kama vile Kwa alinatu na kwengineko.

Kwa mujibu wa maelezo ya watafitiwa walieleza kuwa kazi hii ya upiganishaji wa Majogoo ilikuwa haina msimu bali pale tu yanapopatikana majogoo, na hapo watu huanza kualikana na kusogea katika Mwembe huo nakuanza kupiganisha Majogoo. Kwa shughuli hiyo ndipo lilipozuka jina la Mwembe Majogoo na hadi sasa jina hilo linatumika ingawaje kazi hiyo ya upiganishaji wa Majogoo haipo na huo Mwembe husika umekwisha katwa.

Sambamba na hayo, jina hili la Mwembe Majogoo ni miongoni mwa majina yanayotokana na kanuni ya kimofofonolojia iliyojikita katika uyeyushaji pamoja na muambatano wa maneno mawili yenye kufanya kazi kama nomino.

Ukilichunguza kwa undani zaidi neno hili Mwembe utagundua kuwa limefanyiwa mchakato wa uyeyushaji kwa vile umbo la ndani la neno Mwembe ni / Mu + embe/ kwa kuwa irabu u katika neno hili imefuatiwa na irabu isiyofanana nayo basi irabu

ya juu hiyo imelazimika kupokea mabadiliko na kuwa kiyeyusho /w/ na hapo ndipolilipopatikana neno /mwembe/.

Kutokana na kanuni hiyo ya kimofofonolojia irabu ya juu nyuma/u/ huyeyuka na kupokea sura ama umbo la kiyeyusho cha midomo/w/ na iwapo tu ikiwa itafuatiwa na irabu isiyolingana nayo kisifa za kifonetiki na hapo ndipo huzaliwa sauti /w/ na kuunda jina /neno mwembe/ katika umbo lake la nje kama kanuni hiyo inavyonesha.

$$U __ \{+ w\} \; / __ e$$

$$\begin{Bmatrix}\begin{bmatrix}+sila\\ +son\text{-}nyuma\\ +nyuma\\ +mviringo\end{bmatrix}\end{Bmatrix} ________ + w \; / ___ \begin{Bmatrix}\begin{bmatrix}+sila\\ +kati\end{bmatrix}\end{Bmatrix}$$

Na kwa upande wa neno Majogoo nalo ukilitazama kwa umakini utagundua kuwa limefanyiwa mchakato wa uambikwaji wa kiambishi awali cha wingi /ma/ nakulifanya neno Jogoo kusomeka Majogoo ambalo lipo katika hali ya wingi.Mbali na kanuni ama michakato hiyo jina la mtaa huu limefanyiwa pia mchakato wa uambatishaji kwani nomino mbili Mwembe na Majogoo yamewekwa pamoja na kuunda jina moja “Mwembemajogoo” ambalo hadi sasa lipo na linatumika na wakaazi wa eneo hilo.

Hivyo basi tunaona kuwa jina hili limeakisiwa kutokana na ndege ajulikanaye kwa jina la Jogoo pamoja na shughuli iliyokuwa ikifanyika chini ya Mwembe huo pamoja

na kwamba nadharia jumuishi ilitumika na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa katika uteuzi wa jina la mtaa huo kwani utambulisho wa sehemu hiyo ililenga katika desturi za jamii husikaambazo ziliweza kufanikisha kuibua jina la Mwembe Majogoo.

### 4.2.4 Uteuzi wa jina la mtaa wa Mwembe Punda

Mwembe Punda ni miongoni mwa mitaa mikongwe iliyokuwepo kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ya(1664). Mtaa huu unapatikana katika kijiji cha Ndijani kilichopo Wilaya ya Kati, Mkoa wa kusini Unguja. Mtaa huo upo umbali wa maili kumi na nne(14 ) ukitokea mjini Unguja,Wakaazi wake ni wa mchanganyiko, wapo waliokuwepo kabla ya Mapinduzi pamoja na wazaliwa wa hapo hapo baada ya Mapinduzi ambao walijishughulisha sana na shughuli za kilimo cha Mihogo na Migomba.

Kutokana na maelezo na maandiko ya watafitiwa walieleza na kuandika kwamba wakaazi wa mtaa huu ni watu wa zamani sana kwani miongoni mwao washiriki wa vita vya kwanza vya dunia vilivyopiganwa mwaka ( 1914 - 1918 ) na baadae kushiriki katika Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa upande wa Magharibi ya mtaa huu umepakana na mtaa wa Ndijani kwa Baniani, Mashariki yake umepakana na mtaa wa Ndijani Bondeni, ambapo Kusini umepakana na mtaa wa Ndijani Kijiuni hata hivyo umepakana na Ndijani Mseweni kwa upande wa Kaskzini. Pamoja na hayo Kijiji cha Mwembepunda kimo ndani ya shehia ya Mwembepunda. Sambamba na hayo watafitiwa walisema kuwa mtaa huu wa Mwembe punda ni wa asili kuliko mitaa mingine ipatikanayo Wilaya ya kati Unguja.

Asili ya kuitwa mtaa huu Mwembepunda kulikuwa na Mwembe mkubwa wa kabila la Punda, Embe hizo ziliitwa Punda kutokana na kuwa zilikuwa hazina thamani na hadhi kama zilivyo Embe nyingine, watafitiwa walieleza kuwa Embe hizo zilipewa sifa ya Punda, kwavile Punda katika jamii ana faida nyingi kwa mwanaadamu lakini thamani yake ni ndogo kwa kukosa bahati ya matunzo yake baada ya kazi na tume za mchana kutwa kwa bwana wake,hivyo ni sawa na Embe hizo zilifananishwa na hadhi ya mnyama huyo kwavile hapo zamani zilitumika kama kiungo cha kupikia mchuzi tu na kukosa hadhi ya kutunzwa na kuuzwa sokoni kwa thamani kubwa kama zilivyo Embe za Boribo.

Ukiliangalia jina la Mwembepunda utagundua kuwa mchakato wa kimofofonolojia umetumika katika kuliunda jina hilo kwani kanuni ya uyeyushaji imetumika katika kulikokotoa umbo la ndani la ambalo ni /Mu + embe / na kuwa / Mwembe/ kwa vile irabu / u/ juu nyuma mviringo katika neno/mụ + embe/ imebadilika na kupokea umbo la kiyeyusho cha midomo /w/ kwavile irabu hiyo imefuatiwa na irabu isiyofanana nayo ambayo ni irabu kati mbele /e / na kupatikana neno la umbo la nje / mwembe/ umbo ambalo limekosa irabu /u/ ambayo ilikuwemo katika umbo la ndani la neno hilo kutokana na kanuni hiyo ya kimofofonolojia ya uyeyushaji kama linavyoonesha hapo chini.

U _________ {+ W} / ______ e

{ +Sila, +Son, +Nyuma, +Mviringo } +Kati ____ + W ____ { +Sila, -Nyuma }

Kanuni hii inatwambia kuwa irabu ya juu nyuma /u/ huyayuka na kupokea umbile la nusu irabu / kiyeyusho cha midomo /w/ iwapo irabu hiiyo itafuatiwa na irabu itakayotofautiana nayo kisifa za kimatamshi kama ilivyo irabu kati mbele /e/ katika umbo la neno /Mu + embe/.

Sambamba na hayo jina Mwembe punda limeundwa pia kwa mchakato wa muambatano kwani Nomino “Mwembe” na “Punda” zimeunganishwa kwa pamoja kutokana na kanuni hiyo ya miambatano na kuunda jina moja tu la mtaa huo.

Hata hivyo jina hili la Mwembe Punda limeendana na historia pamoja na matokeo ya sehemu husika nakuthibitisha na maelezo ya watafitiwa kuwa majina mengi ya mitaa hutolewa kwa mujibu wa historia au matokeo, matendo au hata sifa za eneo husika.Sambamba na hayo nadharia ya semiotiki iliweza kumsaidia mtafiti katika kuyachambua maelezo ya watafitiwa kwa kuhusisha jina la mtaa huu na maana ya fasili ya ishara mbalimbali katika lugha nakupelekea uibukaji wa jina la mtaa wa Mwembepunda.

### 4.2.5 Utoaji wa jina la Mtaa wa Kiunga Ndege

Kiunga Ndege ni miongoni mwa mitaa ya kihistoria katika Shehiya ya Ndijani Mseweni, Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja. Ukitokea mjini Unguja hadi ulipo mtaahuu ni umbali wa maili kumi na tatu (13).

Mtaa wa Kiunga ndege unapatikana katikati ya Kijiji cha Ndijani ambapo kaskazini mwa mtaa huu umepakana na Skuli ya Ndijani, ilihali Kusini yake umepakana na mtaa wa Ndijani maweni, Kwa Mashariki umepakana na Ndijani kwa Baniani, hata

hivyo upande wa Magharibi mtaa wa Kiunga ndege unatizamana na mtaa wa Maskani buli. Sambamba na hayo Kiunga Ndege ni mtaa unaokaliwa na wakaazi wengi ukulinganishwa na mitaa mingine ipatikanayoNdijani.

Asili ya wakaazi wa Ndijani Kiunga Ndege ni watu kutokea Kisiwani Charawe kilichopo kusini Unguja, kwa kulithibitisha hilo watoa taarifa wa utafiti huu wameeleza kuwa watu wa Charawe asili yao ni watu waliotokana na kundi la “seven brother of Ali Hassan” ambao walihamia sehemu tofauti za Kisiwa cha Unguja, zikiwemo Unguja Ukuu, Kidoti, Unguja mjini na Charawe.

Pamoja na hayo watoa taarifa waliendelea kutoa maelezo kwa kusema kuwa kundi hilo la watu lililopata nafasi ya kuhamia Charawe ndilo kundi lililosambaa na kuingia Ndijani na kuweka makaazi ya kudumu katika sehemu ya Kiunga Ndege na kujishughulisha na kilimo cha mihogo, migomba pamoja na upigaji wa ndege katika uwanda huo, uzoelekaji wa shughuli hizo kwa wakaazi ulipelekea wakaazi hao kuyapendamandhari hayo kutokana na ardhi yake kukubaliana na vipando walivyokuwa wakiviotesha, na hapo ndipo walipoamua kuhamishia makaazi yao ya kudumu katika sehemu hiyo na kuendeleza harakati zao za upigaji ndegeambapo hapo ndipo lilipopatikana jina la mtaa wa Ndijani Kiungandege.

Jina hili la Kiungandege linatokana na maneno mawili yaliyofanyiwa mchakato wa miambatanisho ambapo neno“unga” lenye maana ya kuweka kitu pamoja na neno “ ndege” ambao walikuwa wakiwindwa na watu hao, sambamba na mchakato huo pia jina hili limefanyiwa mchakato wa uwambishaji kwa kuongezwa kiambishi “KI” mwanzoni mwa neno “unga” na kupatikana neno “kiunga” lenye kubeba maana ya

sehemu ya uwanda (isiyo na kitu zaidi ya mwitu) na kuunganishwa na neno “Ndege” na hapo ndipo likapatikana jina la mtaa Kiungandege.

KANUNI

**Ki + Unga + Ndege _________ Kiungandege.**

Kutokana na maelezo na maandiko ya watafitiwa tunaona wazi kuwa uteuzi wa jina hili la Kiungandege unatokana na uhusiano mkubwa wa shughuli za kijamii na kiuchumi zilizokuwa zikifanywa katika sehemu hiyo ambapo wengi wa watoa taarifa walieleza kuwa wahamiaji kutoka Charawe walijishughulisha na shughuli hizo za kilimo na upigaji wa ndege katika sehemu hiyo na ndipo likapatikana jina la mtaa wa Kiungandege. Hata hiyo uteuzi wa jina la mtaa huu umesadidu kwa kulingana na nadharia jumuishi ambayo imejikita zaidi katika katika utambulisho wa jamii husika kwa kulingana naharakati zao za kiuchumi na kijamii.

### 4.2.6 Uteuzi wa Jina la mtaa wa Kicheche

Kicheche ni mmoja wapo kati ya mitaa ya zamani iliyomo katika Wilaya ya Kaskazini “A” Mkoa wa Kaskazini Unguja shehiya ya Mkokotoni. Mtaa wa Kicheche upo umbali wa maili ishirini na saba (27) kutokea mjini Unguja.

Asili ya watu wa Kicheche ni kutoka Kilindi Nungwi iliyopo Kaskazini mwa Unguja.Watoa taarifa wengi akiwemo Mzee Ali Juma Juma wanaeleza kuwa watu wa mwanzo kuhamia katika mtaa huo  alikuwa babu yake mzaa Baba aliyekuwa akifahamika kwa jina la Mzee Juma Juma Tembea tangia  vita vya pili vya dunia

(1939 - 1945) yasemekana  Mzee huyo alitokea Kilindi akiwa na familia yake na kuweka makaazi yake ya kudumu katika eneo hilo.

Asili ya jina la Kicheche linatokana na tabia za kuhamahama za Mzee Juma Tembea kukimbia viambo na kuishi mwituni mbali na jamii, tabia hizo zilizofananishwa na zile za mdudu aitwae Cheche ambae anaishi porini mbali na vinyama vingine vinavyolingana na yeye.

Kwa mujibu wa maandiko na maelezo ya watafitiwa walisema kuwa kipindi hicho alichofika Bwana Juma kulikuwa na pori tupu ndipo alipolima na kufyeka pori hilo na kufanya makaazi yake ya kudumu yeye na familia yake  na kupaita jina la Kicheche.  Mzee huyu pamoja na familia yake baada ya kuwasili na kuishi katika eneo hilo alijishughulisha na kazi za utengenezaji wa waya za simu za Waingereza, alifanya biashara za kukodi Minazi pamoja nakuuza mbata, sambamba na hayo mzee huyo alikuwa mkulima wa mihogo na kunde na aliotesha miti tofauti kwa vile alifika sehemu ambayo ilikuwa mpya kimakazi, miti hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya kuimarisha mtaa wake mpya.

Mtaa wa Kicheche umepakana na mitaa  ya Utaani, Misufini na Kiongele kwa upande wa kusini, kwa upande wa kaskazini kuna bahari ya tumbatu pamoja na mto Chaamani. Hata hivyo Mashariki mwa Kicheche kumepakana na mto mkubwa wa Mibuyuni na kwa magharibi umepakana na Chemchem  ya maji baridi ambayo ndio yaliyokuwa yakitumika kwa kunywa na kupikia kwa kipindi hicho.

Hivyo ukiliangalia kwa umakini jina la mtaa wa Kicheche utagundua kuwa mchakato wa kimofolojia umefanyika kwa kuambatanisha kiambishi “ki” mwanzoni mwa neno“cheche” na kusababisha jina la mtaa huo kuitwa Kicheche

**“ki” +mzizi wa nomino (cheche)-----------jina kamili Kicheche.**

Kutokana na maelezo na maandiko ya watafitiwa yanadhihirisha wazi kuwa jina la mtaa huu limetolewa kutokana na kufananishwa tabia za muanzilishi na muasisi wa mtaa huo ambae ni mzee Juma wa Juma Tembea zinafanana na mdudu Cheche kutokana na kupenda kuishi porini.

Hivyo basi hii inadhihirisha wazi kuwa jina hili limeteuliwa kwa kuzingatia maana za isharra ambayo ni msingi wa nadharia ya semiotiki ambao ulitumika katika uibukaji wa jina la mtaa wa Kicheche, pamoja na hayo inadhihirisha kuwa mengi ya majina ya mitaa hufanyika ama huundwa kwa kutumia kanuni za Kimofolojia.

### 4.2.7 Uteuzi wa Jina la Mtaa wa Mwembepopo

Mwembepopo ni miongoni mwa mtaa uliomo ndani ya Shehia ya Bumbwini Makoba katika Wilaya ya Kaskazini “B” Unguja, inakadiriwa kuwa mtaa wa Mwembepopo upo umbali wa maili kumi na nane (18) kutokea mjini Unguja. Mtaa huu umepakana na mitaa kadhaa kama vile mtaa wa Mbuyuni kwa upande wa kaskazini, mtaa wa Vidugu upande wa kusini, ama kwa upande wa mashariki mtaa huu umepakana mtaa wa Mwembe mazizi pamoja na mtaa wa Udodoudugu ambao unapatikana upande wa magharibi mwa mtaa wa Mwembe popo.

Asili ya watu wa mtaa huu ni Watumbatu ambao wamefika hapo zaidi kwa shughuli za kilimo na uvuvi .na ndipo vijanawaliokuwa wakiongozwa na kiongozi aliyekuwa akijulikanwa kwa jina la (mudiri) vijana hao walikuwa wakienda sehemu hiyo kupiga popo hao kwa ajili ya chakula, hivyo kutokana nahali hiyo ndipo wahamizi hao wakauita mtaa huo Mwembepopo.Ingawaje watu wengine waliuita mtaa huo kwa jina la (Mdodotunga), kutokana na kwamba popo walikuwa wakitunga na kisha kutunguliwa kwa mawe kupitia panda (manati).

Kwa upande mwengine jina la Mwembepopo limetokana na kanuni ya kimofofonolojia. Kwa vile kanuni ya uyeyushaji imetumika kutoka umbo la ndani la neno Mu + embe na kuwaMw + embe kwa vile irabu ya juu / U/ katika neno Mu + Embe imefuatiwa na irabu isiyofanana nayo kisifa ambayo ni irabu kati / E / na kupelekea irabu /U/ kupokea badiliko na kuwa kiyeyusho /W/ cha midomo na kuzalika neno /mwembe/ katika umbo la nje.Kama inavyoonesha kanuni ya jumla hapo chini.

U ________ {+ W} / ______ E

{ +Sila, +Son, +Nyuma, +Mviringo } → { +Kati, ____ + W } / ____ { +Sila, -Nyuma }

Kanuni hii inatufafanulia kuwa iwapo irabu ya juu nyuma /U/ ikifuatiwa na irabu ya kati mbele /E/ katika umbo la ndani basi irabu hiyo ya juu nyuma /U/ hupokea badiliko na kuwa katika sura ya kiyeyusho cha midomo /W/.

Sambamba na hayo jina hili limetokana na kanuni ya mofolojia ya muambatano kwa vile nomino mbili kati ya mwembe na popo zimeshikanishwa pamoja na kuunda jina moja ambalo ni Mwembepopo.

Hivyo basi kutokana na maelezo na maandiko ya watafitiwa tunaona kuwa jina hilo limesadifu kutokana na hali halisi ya matokeo na matendo yaliyokuwa yakifanyika katika sehemu hiyo ambayo yalijumuisha ujio wa  Popo katika mwembe pamoja na mawindo ya wakaazi wa asili wa mtaa huo. Hata hivyo nadharia jumuishi imemsaidia mtafiti katika kuzipambanua data hizi kwa kuzihusisha na utambulisho wa sehemu husika nashughuli zilizokuwa zikifanyika katika eneo hilo ambalo ndilo lililopelekea uibukaji wa jina la mtaa wa Mwembe popo.

### 4.2.8 Uteuzi wa Jina la Mtaa wa Kisima Majongoo

Mtaa huu ni miongoni mwa mitaa ya zamani sana ambayo Waafrika wa makabila tofauti waliishi hapo. Kisimamajongoo ni mtaa uliopo katikati ya Unguja mjini katika Wilaya ya Mjini Mkoa MjiniMagharibi, Shehiya ya Kisimamajongoo.

Mtaa huu upo katikati baina ya mtaa wa Michenzani, Kisiwandui na Kikwajunibondeni.Watu waliokuwa wakiishi katika mtaani hapo ni kutoka makabila tofauti ya Tanzania bara wakiwemo Wandengereko, Wazaramu,Waruguru na hata Wanyasa.

Asili ya kuitwa Kisimamajongoo kulikuwa na kisima katikati ya eneo hilo ambacho kimezungukwa na majongoo  pembezoni mwake na ndipo wakaazi waliokuwa wakiishi karibu na eneo hilo wakakiita Kisima hicho kuwa ni kisima cha  majngoo

kutokana na kuwa majongoohayo yalivyokizunguka kisima hicho na hapo ndipo wakaazi wa eneo hilo walipovumbua jina la mtaa wa Kisimamajongoo.

Wakaazi wa mtaa huu walikuwa wakulima na wafanyakazi katika ofisi za serikali, pamoja na kujishughulisha na biashara za mboga mboga kama vile kisamvu, mronge,maandazi na vitumbua. Kisima hicho kilikuwa kikitumika kwa ajili ya maji ya kunywa ambapo maji yake yalisifikana kwa ubaridi wa kukata kiu za wakaazi haraka.Ingawaje kisima hicho kwa sasa hakipo na limebaki jina tu la mtaa huo wa Kisimamajongoo. Jina hili la Kisima majongoo limetokana na kanuni ya kimofolojia ya uambatanishaji wa nomino mbili ambazo ni Kisima na Majongoo na kupatikana jina moja la Kisima majongoo.

Vile vile jina hili limefanyiwa mchakato wa uambishaji kiambishi /ki/ chenye kuashiria idadi ya umoja kimeambikwa mwanzoni mwa shina / sima/ na kupatikana neno Ki+sima hata hivyo nomino Jongoo nayo imeambikwa kiambishi /ma/ chenye kuashiria wingi mwanzoni mwa nomino hiyo na kuunda neno Ma + jongoo.

Kulingana na mazingira ya mahali hapo, watafitiwa wameeleza kuwa jina hilo limesadifiana na mazingira yaliyokuwepo katika eneo hilo, hata hivyo nadharia ya semiotiki iliweza kumsaidia mtafiti katika kuzichanganua data hizo kwa kutoa maana ya fasili kwa kulenga ishara ambapo moja kwa moja ishara hizo zililenga majongoo yaliyokizunguka kisima hicho na ndipo kukapatikana jina la Kisimamajongoo.

### 4.2.9 Uteuzi wa jina la Mtaa wa Mlandege

Mtaa wa Mlandege ni mtaa uliomo katika Wilaya ya Mjini Mkoa wa MjiniMagharibi katika mitaa ya Kwahajitumbo, Mchangani,Barastekipande na Mchambawima ambapo kutokana na maelezo na maandiko ya watafitiwa watu wa mitaa hii ni wenye asili za makabila tofauti kutoka Tanzania Bara wakiwemo Wazaramu,Wanyamwezi na Wanyakusa.

Asili ya kuitwa mtaa huu Mlandege kulikuwa kuna mti mkubwa ambao walikuwa huja ndege tofauti na kula tunda zake pamoja na kufyonza maji yanayotoka katika maua ya mti huo na ndipo wakaazi wa hapo walipoliibua jina la pahali hapo kwa kupaita Mlandege,kutokana na shughuli walizokuwa wakizifanya ndege juu ya mti huo.Wengi wa watafitiwa walisema kuwa mti huu ulikatika zamani sana na kubaki jina la Mlandege tu ambalo imekuwa athari ya matokeo hayo.

Hivyo basi nadharia jumuishi ilimsaidia mtafiti katika kuyachanganua maelezo ya watafitiwa kwa kuitambulisha jamii kutokana na maelezo na maandiko ya watafitiwa tunaona kuwa mitaa mingi ya Unguja hutokana na suala zima la utambulisho ambao aidha hutokana na historia, mila, desturi au hata kitendo ambacho hufanyika katika eneo husika.

## 4.3 Mahusiano ya Maana ya Majina ya Mitaa na Majina ya Wadudu, Wanyama na Ndege

Mtafiti katika kupata data kwa ajili ya kukamilisha utafiti wake huu alitumia mbinuya hojaji, mahojiano pamoja na ushuhudiaji na taarifa alizozipata zilikuwa faafu kwani ziliweza kujibu swali la pili na la tatu la utafiti huu, kutokana na majibu

na taarifa za watafitiwa zilieleza kuwa majina mengi ya mitaa yalihusishwa na maana ya matukio mbalimbali ya kihistoria yaliyokuwa yanatokea katika mitaa hiyo.

Zubeir (2015) alitafiti kuhusiana na Etimolojia ya Kaskazini Pemba kuwa utambulisho wa utamaduni wa Wapemba. Katika tafiti hii aliweza kubaini kuwa majina mengi yanayotolewa katika Mkoa wa Kaskazini mwa kisiwa cha Pemba huwa na mahusiano ya kutambulisha utamaduni wa Wapemba.

Naye Schosman (2003) alitafiti kuhusu majina ya vituo vya daladala na mitaa ya Dar es Salaam.Katika utafiti wake huo aliweza kugundua mahusiano yaliyopo baina ya vituo vya daladala na majina ya mitaa na kuendelea kusema kuwa majina hayo yanaweza kuwa na uhusiano wa matukio ya kihistoria yaliyokuwa yakifanyika katika mitaa hiyo.

Kwa kutumia njia ya hojaji, mahojiano na ushuhudiaji watafitiwa wa kisiwa cha Ungujia waliweza kubainisha kwamba mahusino ya maana ya majina ya mitaa jinsi yanavyoweza kuhifadhi mila,tamaduni nahata historia ya matukio muhimu yaliyoweza kutokea katika mitaa husika ambapo hali zote hizo zilizingatia shughuli za kiuchumi na kijamii ambazo zilikuwa zikifanywa katika mitaa husika.

### 4.3.1 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kiziwandege

Tukiangalia jina la mtaa wa “KIZIWA NDEGE=” ambalo mtafiti alifanikiwa kulitafiti na kufanikiwa kupata taarifa kutoka kwa watafiti wake yakuwa, jina hili lilihusishwa na mfumo mzima wa harakati za kilimo cha mpunga zilizokuwa zikifanyika katika eneo hilo,pamoja na ndege ambao waliokuwa wakija kwa ajili ya

kufata maji pamoja na mpunga huo kwa ajili ya chakula chao katika eneo hilo. Pamoja na hayo nadharia jumuishi ilihusika katika uchanganuzi wa data hizi kwani nadharia hii imejikita zaidi katika kueleza utambulisho wa jamii ya wakaazi wa mtaa huo pamoja na harakati zao za kimaisha.Hivyo mahusiano hayo ndiyo yaliyoibua jina la Kiziwandege.

### 4.3.2 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kisimang'ombe

Vile vile kwa upande wa mtaa wa "KISIMA NG'OMBE" watoa taarifa wengi kuhusu mtaa huu walieleza kuwa jina hili limetokana na mahusiano ya kimaana baina ya Ng'ombe na Kisima, ambapo Ng'ombe hao walikuwa wakipelekwa hapo kwa ajili ya kupatiwa chanjo ikiwa ni miongoni mwa huduma za kiafya kwa wanyama hao,mahusiano hayo ndiyo yaliyopelekea kuibuka jina la Kisima Ng'ombe. Pamoja na hayo nadharia ya semiotiki ilifanikisha katika uchambuzi wa data hizo ambapo nadharia hiyo imejikita zaidi katika kutoa maana za ishara mbalimbali katika lugha, yakiwemo majina ya watu, vitu na hata mitaa.

### 4.3.3 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Mwembemajogoo

Hata hivyo kwa upande wa jina la mtaa wa "MWEMBE MAJOGOO" nalo mtafiti kupitia watifi wake alibaini kuwa jina hili limeteuliwa kutokana na mahusiano ya kimaana yaliyopo baina ya Mwembe na Majogoo pamoja na shughuli ambazo zilizokuwa zikifanyika hapo, ambazo ndizo zilizochangia kuibua jina la Mwembe Majogoo. Kwavile watoa taarifa wengi walidai kuwa katika eneo hilo kulikuwa na harakati za kupiganishwa majogoo chini ya mwembe, sambamba na hayo nadharia jumuishi ilimsaidia mtafiti katika kuchanganua data alizozipata kutoka uwandani kwani nadharia hii imejikita katika kutoa utambulisho wa jamii husika kutokana na

harakati zao za kimaisha, na ndio maana mtaa huo hadi leo unaitwa kwa jina hilo kutokana na harakati hizo ingawaje kwa sasa harakati hizo hazifanyiki.

### 4.3.4 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Mwembepunda

Kwa upande wa jina la mtaa wa “MWEMBE PUNDA” mtafiti aligundua kuwa jina hilo lilihusishwa moja kwa moja kimaana na embe zitokanazo na mwembe huo ambazozilionekanwa kuwa hazina thamani kuliko aina nyingine za embe kama ambavyo anavyochukuliwa mnyama Pundaambaye anatumika sana lakini thamani yake ni ndogo katika maisha halisi ya binaadamu ukimlinganisha na wanyama wengine wakiwemo Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo na Ngamia, ambao wamelingana naye kiumbile na kimakaazi, kwa minajili hiyo embe za mwembe huu zinatumika kwa ajili ya kiungo tu katika mchuzi, sifa ambayo ilifananizwa na sifa ya mnyama Punda ambae hutumika kwa ubebaji wa mizigo tu nasi kwa matumizi mengine kama vile kitoweo, hivyo kutokana na uhusiano wao huo wakithamani ndio uliochangia kuibuliwa kwa jina la “Mwembe Punda” ambalo hadi leo lipo na linatumika. Hata hivyo nadharia ya semiotiki ilimsaidia mtafiti kupata undani wa jina la mtaa huo kwa vile nadharia hiyo imejikita katika kutoa maana kwa ishara katika lugha ambapo jina hili lilihusiana zaidi kimaana na mnyama punda kutokana na harakati zake.

### 4.3.5 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kiungandege

Nalo jina la mtaa wa “KIUNGA NDEGE” watoa taarifa wengi walidai kuwa jina hililinahusiana na shuguli za kiuchumi ambapo wakaazi wa eneo hilo walijishughulisha na kilimo cha choroko katika eneo la uwanda ambalo lilikuwa ni kama eneo la makutano ya ndege wa aina tofauti ambao walikuwa wanakutana hapo kwa ajili ya kujipatia chakula kupitia choroko zilizokuwa zinaoteshwa na wakaazi

wa eneo husika, hivyo kutokana na makutano ya ndege hao katika eneo hilo ndipo wakaazi wa eneo hilo wakaamua kupaita kiunga ndege pahala hapo jina ambalo limebuniwa kutokana na mahusiano ya kimatendo yaliyokuwa yakifanyika hapo. Kwavile neno "Kiunga" linabeba maana ya uwanda wenye kuunganisha na kukutanisha na neno "ndege" linamaanisha jamii ya ndege tofauti waliokuwa wanafika katika eneo hilo, hivyo kutokana na muungano wa ndege hao katika eneo hilo ndipo wakaazi wa eneo hilo walipoibua dhana na kuhusisha eneo hilo na kazi ya kuwaunganisha ndege hao, na hapo ndipo likaibuka na kuzuka jina la mtaa wa kiunga ndege ambalo linatumika hadi na wakaazi wa sasa. Kwa vile nadharia jumuishi inajikita zaidi katika kutoa utambulishowa jamii pamoja na harakati za kiuchumi na kijamii katika mfumo mzima wa maisha.

### 4.3.6 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kicheche

Kwa upande wa uteuzi wa jina la mtaa wa "KICHECHE" mtaa ambao unapatikanwa Kaskazini mwa kisiwa cha Unguja, watoa taarifa wa mtaa huu walidai kuwa jina hili lina mahusiano ya karibu ya kimaana na mduduaitwaye"Cheche" kwa vile mdudu huyuana tabia za kuishi msituni na hapendi kujichanganya na wadudu wengine waliotofauti na kabila lake, tabia ambazozilihusishwa na tabia za wakaazi wa awali waliofika na kuishi katika eneo hili kwavile wakaazi hao walikuwa na tabia kama za mdudu huyo za kuhama sehemu ambazo wanaishi watu wa makabila tofauti na wao na kuhamia sehemu ambayo haina watu kwa matarajio ya kuishi pekeyao bila kujichanganya na makabila mengine, hivyo kutokana na uhusiano wa tabia hizi hapo ndipo iliposadifu na kutolewa jina la mtaa huo kuwa ni mtaa wa vicheche yaani mtaa wa watu wa kuhamahama kwa lengo la kujitenga na kujibaguwa na jamii nyingine za

watu kimakaazi. Hata hivyo jina hili linaonesha wazi kuwa limetolewa kwa kuangalia maana za ishara katika utoaji wa majina kama inavyojidhihirisha katika nadharia ya semiotiki.

### 4.3.7 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Mwembepopo

Nao uteuzi wa jina la mtaa wa "MWEMBE POPO" mtaa ambao unapatikana katika kijiji cha Bubwini kilichopo kaskazini mwa kisiwa cha Unguja,wengi kati ya watoa taarifa kuhusu mtaa huu walisema kuwa jina la mtaa huo lililohusishwa kimaana baina ya Mwembe uliokuwapo katikati ya kitongoji cha Bumbwini na ujaji wa "Popo" waliokuwa wakitua juu ya mwembe huo kwa ajili ya kupumzika wakati wa mchana baada ya mahangaiko yao ya usiku kucha lengo la kujitafutia chakulakwa, na kwavile viumbe hawa ifikapo wa wakati wa mchana hupungua nuru ya kuona ndipo wanapokuja na kupumzika katika mwembe huo na hapo ndipo wakaazi wa mtaa huo walipouhusisha mwembe huo na zile tabia za popo hao za kuja kupumzika na kuchangia kuibuliwa kwa jina la mtaa wa"Mwembe popo" kutokana na matendo hayo. Kwa upande wa uchambuzi huu nadharia jumuishi ilimsaidia mtafiti katika kukamilisha uchambuzi wake kwa kugundua utambulisho wa wakaazi wa mtaa husika.

### 4.3.8 Mahusiano ya maana ya jina la Mtaa wa Kisimamajongoo

Kwa kuendelea na uteuzi wa jina la mtaa wa "KISIMA MAJONGOO" kupitia watoa taarifa, mtafiti aligundua kuwa uteuzi wa jina la mtaa huu nalo limetokana na mahusiano ya kimaana iliyopo baina ya Majongoo yaliyokuwa yamekizunguka Kisima ambacho kilikuwa kinapatikanwa katika eneo hilo na kilitumiwa na wakaazi wa mtaa huo kwa ajili ya kupata maji, hivyo sifa ya jina la mtaa huo na hapo ndipo

likazuka jina hilo kuwa huu ni mtaa wa kisima majongoo kutokana na uwepo wa majongoo hayo katika kisima hicho ambacho hivi sasa hakipo bali jina la mtaa limebaki na linaendelea kutumika kwa wakaazi wa mtaa huo pamoja na wakaazi wa Unguja kwa ujumla wake. Hata hivyo nadharia ya semiotiki ilimsaidia mtafiti kuibua maana ya jina la mtaa huo kwa kuchunguza ishara zilizolenga katika jina hilo.

### 4.3.9 Mahusiano ya kimaana ya jina la Mtaa wa Mlandege

Kwa kumalizia na utoaji wa jina la mtaa wa "MLANDEGE" watoa taarifa wa mtaa huu walisema kuwa uteuzi wa jina hili umetokana na uhusishwaji wa tabia za ndege wa aina ya Misese, Kunguru, Mnana pamoja na Ninga, ndege ambao walikuwa wakija mtaani hapo na kutua katika Mti uliokuwa unapatikana mtaani hapo kwa lengo la kuja kula tunda zilizokuwa zikipatikana katika mti huo hivyo mahusiano ya ndege hao juu ya mti huo ndipo Wakaazi wa eneo hilowalipoliibua jina la Mlandege jina ambalo linatumika hadi hivi leo ingawa mti wenyewe pamoja na ndege hao wametoweka kwa sasa. Sambamba na hayo maelezo hayayalijikita zaidi katika nadharia jumuishi kwani uwepo wa ndege hao pamoja na matendo yao ni utambulisho tosha juu ya uteuzi wa jina la mtaa huo.

Kutokana na hali hizo tumebaini kuwa mahusiano ya maana ya majina ya mitaa yamehusishwa zaidi na mfumo mzima wa utoaji wa fasili za maana zinazolenga ishara mbalimbali katika lugha, sambamba na kuhusisha matukio ya kihistoria, kiutamaduni,kimila na hata harakati mbali mbali katika mfumo mzima wa maisha ya mwanaadamu pamoja na mazingira yaliyomzunguka. Ambapo hiyo ndiyo misingi mikuu ya nadharia ya semiotiki na nadharia jumuishi ambapo mtafiti alizitumia

nadharia hizi na zilimuwezesha kujibu suali lake la pili sambamba na kutumia mbinu ya hojaji, na mbinu ya mahojiano katika kukamilisha utafiti wake huo.

## 4.4 Sababu Zinazochangia Majina ya Wanyama, Ndege na Wadudu Kuakisiwa na Majina ya Mitaa

Mchakato wa utoaji wa majina ni tukio la kijamii na kiutamaduni lenye kuonesha historia ya jamii husika,pia majina husimamia tajriba ya mtu au kikundi cha watu, mila, desturi, hadhi na mamlaka katika jamii (Guna, 2001).Hivyo basi majina ya watu, mahala na hata ya mitaa hubeba utambulisho wa jamii husika nakuitafautisha na nyingine, hata hivyo huweza kutafautisha baina ya mtu au mtaa mmoja na mwengine. Kwa muktadhakama huu ni dhahiri kuwa majina ya wanyama, ndege na wadudu huweza kuakisiwa na utoaji wa majina ya mitaa kutokana na sababu mbalimbali.

Hivyo, mtafiti kupitia mbinu ya ushuhudiaji ameweza kubaini sababu hizo na kuweza kujibu swali la tatu la utafiti huu.Ambapo ilimpelekea mtafiti kugundua sababu kadha wa kadha zinanazochangia majina ya wanyama ndege na wadudu kuakisiwa na utoaji wa majina ya mitaa, zikiwemo; sababu za kihistoria,kimila nakiutamaduni ambazo tamaduni hizo huhusisha suala zima la shughuli za kiuchumi wa mtaa husika, vile vilena mtafiti amebaini kwamba majina ya mitaa hiyo mingi yao hupewa majina kutokana na sifa ama tabia zilizo husishwa ama kufananishwa moja kwa moja na sifa, tabia ama matendo ya wanyama, ndege au wadudu ambao watakuwawamehusika ama kupatikanwa katika eneo ama mtaa husika ulipo.Taarifa hizi zinakwenda sambamba na nadharia ya semiotiki na nadharia jumuishi ambazo zinajikita katika kutoa fasili za maana ya ishara mbalimbali katika lugha, pamoja na

kujikita katika utambulisho wa jamii husika katika majina ya mitaa kulingana na historia, mila, utamaduni na harakati za kiuchumi na kijamii, ambazo zilipelekea uteuzi wa majina ya mitaa kwa kupitia majina ya wanyama, ndege na wadudu.

## 4.5 Muhutasari wa Sura

Sura hii imeangazia uchambuzi wa data ambazo zilikusanywa uwandani, data ambazo zimechambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo ambao umeenda sambamba na malengo pamoja na maswali ya utafiti, na kuelezea namna majina ya wanyama ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa katika utoaji wa majina hayo. Sura inayofuata ni muhutasari, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaonesha muhtasari hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Ambapo mtafiti alichunguza majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa, na kugundua kwamba majina ya mitaa hiyo hutokana na historia, tamaduni ama mila za wakaazi wa mitaa husika. Pamoja na kutoa mapendekezo kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilihusu kuchunguza majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa.Ambapo lengo hili lilifanikiwa kutokana na taarifa tulizozikusanya kupitia malengo mahususi ya utafiti huu ambayo ni: Kubainisha majina ya wanyama, ndege na wadudu yanvyotumika kuwakilisha majinaya mitaa, kuainisha mahusiano ya maana ya majina yamitaa na majina ya wadudu, wanyama na ndege na kuchambua sababu zinazochangia majina ya mitaa kuakisiwa na majina ya wanyama, ndege na wadudu.

Hata hivyo data za majibu hayo zilichanganuliwa kwa namna ya kuweza kuonesha sababu, mahusiano ambayo yaliyoweza kupelekea majina hayo ya wanyama, ndege na wadudu kuibua majinaya mitaa, vile vile uchanganuzi huo uliongozwa na nadharia ya Semeotiki ambayo ilitumika kuonesha uchanganuzi wa lengo la kwanza na la pili la utafiti huu, pamoja na kumalizia kwa nadharia Jumuishi iliyokuja kukamilisha lengo la tatu la utafiti huu.

### 5.2.1 Matokeo ya lengo la kwanza la utafiti

Lengo la kwanza la utafiti huu ni kubainisha majina ya wanyama, ndege na wadudu yanayotumika kuwakilisha majina ya mitaa.Ambapo lengo hili lilimuwezesha mtafiti katika kujibu suali la kwanza la utafiti huu lisemalo: Ni majina yepi ya wanyama yanayotumika kuwakilisha majina ya mitaa?Kutokana na lengo hilo mtafiti aliweza kubaini kwamba kuna majinaya wanyama, ndege na wadudu, ambayo yanaakisiwa katika kuwakilisha uteuzi majina ya mitaa na matokeo ya utafiti huu ni kwamba, kuna Wanyama, Ndege na Wadudu tofauti kama vile Kuku, Punda, Jongoo, Ng'ombe, Popo, Cheche, Mbuzi, Chui, Paa viumbe hivyo mtafiti amebaini ya kuwa majina yao hutumika katika uteuzi wa majina ya mitaa kutokana na tabia zao, mazingira husika ama shughuli za kijamii ambazo ziliunganishwa na wanyama, ndege na wadudu katika maeneo hayo kulingana na kazi za kiuchumi na kijamii za wakaazi wa eneo husika. Kutokana na lengo pamoja namatokeo ya lengo hilo kuna nafasi ya kutosha kwa wataalamu katika kuliziba pengo la utafiti huu kwa kuangazia uchunguzi wa majinaya miti au hata viumbe vya baharini katika uteuzi wa majina ya mahala na mitaa. Kwa upande wa watunga sera waunganishe maalumati haya katika kuhifadhi, kukuza mitaala ya kielimu kwa kuekea kumbukumbu kwa watunza mitaala ya kielimu, wanazuoni, walimu wa shuleni na watafiti.Vile vile tukio la utoaji wa jina la mtaa au mahali ni fursa ya wanajami wa eneo husika kwani wao ndio wanoifahamu na kuiyelewa vyema historia ama tamaduni ya sehemu wanayoishi, Hivyo wana jamii wanafursa nzuri ya kuibua na kuwasilisha majina ya mitaa ya maeneo yao husika.

### 5.2.2 Matokeo ya Lengo la pili la Utafiti

Matokeo ya lengo la piliKatika tafiti hii ambalo lililenga: Kubainisha mahusinao ya kimaana ya majina ya mitaa na majina ya wadudu, wanyama na ndege. Kupitia lengo hili mtafiti aliweza kujibu suali la pili la utafiti huu lisemalo: Kwa nini majina ya wanyama, ndege na wadudu huakisiwa na majina ya mitaa? Matokeo yakeimebainika kwamba kuna mahusino makubwa ya kimaana baina ya majina ya wadudu, wanyama na ndege na uteuzi wa majina ya mitaa, kwa kawaida mahusino hayo hutokana na mila, historia pamoja natamaduni za eneo husika ambalo hushirikisha harakati za kiuchumi na kijamii zifanyikazo katika mitaa husika. Vile vile mahusiano hayo yamehusishwa namichakato mbalimbaliya kimofofonolojia inayotumika katika kuibua ama kubuni majina ya mitaa itokanayo na majina ya wanyama, ndege na wadudu. Hivyo kupitia lengo hili wataalamu mbali mbali wanao uwezo wa kutumia mwanya huu kwa kuchunguza majina ya mitaa na mahusiano ya kazi zinazofanywa na wanajamii wa eneo husika. Hata hivyo kwa upande wa watumga sera ni nafasi nzuri ya kuunganisha mahusiano haya ya majina ya mitaa na historia ya kisiwa cha Unguja kwa kuikuza na kuiendeleza kumbukumbu ya kisiwa hiki ili iweze kutumika katika mitaala ya kielimu kwa kupitia wanazuoni, walimu wa shule na watafiti wajao.

### 5.2.3 Matokeo ya lengo la tatu la utafiti

Lengo la tatu la utafiti huu ni kuchambua sababu zinazopelekea majina ya wanyama, ndege na wadudu kuakisiwa na majina ya mitaa.Ambapo lengo hili lilienda sambamba na suali la tatu la utafiti huu lisemalo: Sababu zipi zinazochangia majina ya mitaa kuakisiwa na majina ya wanyama, ndege na wadudu? Matokeo ya suali hilo

ni kwamba, mtafiti alifanikiwa kubaini sababu mbalimbali ambazo zinapelekea uibuaji wa majina ya mitaa kutokana na majina ya wanyama, ndenge na wadudu ambapo sababu hizo ni pamoja na zakihistoria, kimila, kiutamaduni na kimazingira, sababu ambazo zimebainika kuwa ndizo zinazopelekea kuwepo utofauti kati ya mtaa mmoja na mwengine. Hivyo matokeo haya kuhusu lengo la tatu la utafiti huu yanatoa fursa adhim kwa watunga sera, wasomi mbalimbali, walimu pamoja na wakuza mitaala ya kielimu pamoja na wanajamii katika kuendeleza historia ya kisiwa hiki, pamoja na kurithisha taaluma hii kutoka kizazi kimoja hadi kingine sambamba na kutoa ushawishi kwa watafiti wajao katika kubaini mwanya wa kiutafiti na kuutafutia ufumbuzi wa kitaaluma.

Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yamegundua kuwa majina ya wanyama, ndege na wadudu kuwa ni kweli majina hayo huakisiwa kwa kiasi kikubwa katika utoaji wa majina ya mitaa. Hivyo basi mtafiti anapendekeza kufanyika kwa tafiti nyingine za majina ya mitaa ambayo yanatokana na miti, mimea na matunda ili kuweza kuongeza misamiati katika lugha ya Kiswahili pamoja na kukuza historia, mila na tamaduni za sehemu husika.

## 5.3 Mapendekezo juu ya Tafiti Zijazo

Maelezo kuhusu majina ya mitaa yameelezwa na watu mbali mbali. Mtafiti amezungumzia kuhusu majina ya wanyama, ndege na wadudu jinsi yanvyoakisiwa na majina ya mitaa katika kisiwa cha Unguja. Mtafiti amebaini kuwa kipengele cha majina ya viumbe vikiwemo vya baharini kama vile samaki, viumbe vya nchi kavu kama vile watu mashuhuri na maarufu, majina ya miti, matunda, ufundi na ubunifu pamoja na matendo ya watu yanafaa kuangaziwa kwa jicho la kiutafiti. Hivyo mtafiti

anapendekeza kuwa vipengele hivyo vinahitaji kuangaliwa kwani vimegundulika kuwa majina kama hayo ni moja wapo ya vipengele vinavyotumika katika uwakisifu wa utamaduni wa jamii pamoja na utoaji na upangaji wa majina ya mitaa. Hivyo imependekezwa kwa tafiti zijazo kujihusisha na athari za majina ya viumbe, vitu pamoja na matendo ya watu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa. Pia athari za kifonolojia, kimofolojia na kisemantikia katika utoaji na upangaji wa majina ya watu pamoja na mitaazifanyiwe utafiti ili kuona jinsi gani wanajamii wanavyoweza kuvitawala vyema vipengele vya kiisimu katika utoaji na upangaji wa majina ya watu na sehemu wanazoishi maishani mwao.

## 5.4 Muhutasari wa Sura

Kwa muhtasari sura hii imetoa majumuisho ya utafiti mzima, muhtasari wa matokeo ya utafiti pamoja na kumalizia na mapendekezo ya utafiti.

**MAREJELEO**

Buberwa, A. (2010). “Investigating of Sociolinguistic Aspect of Place Name in Ruhaya in North West Tanzania.” Unpublished M. A.Dissertation. University of Dar es Salaam.

Bakari, A. (2005). “Makala ya Bakari Abeid.” Baraza la Kiswahili Zanzibar (haijachapishwa).

BAKIZA (2000). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Nairobi: Oxford University Press.

BAKIZA (2008). *Utamaduni wa Mtanzania, Zanzibar.*

Best, J. W. na Kahn, J. V. (1993). *Research in Education*. New York: Ally and Bacon.

Brown, G. (1995). *Speakers, Listeners and Communication, Explanation in Discouse Analysis.* New York: Combridge University Press.

Cameroon, K. (1961). *English Place Names.* London: Exford University Press.

Cohen, L. & wenzake (2000). *Research Methods in Education.* London: Routledge Falmer.

Chum, H. (1982). *Desturi na mila zetu Arusha.* East Africa Publicantion Limited.

Creswell, J. C. (2002). *Education Research: planning, Conducting and Evaluation Quantitative anda Qualitative Research*. USA: Pearson Education.

Enon, J. C. (1998). *Education Research, Startistic and measuremnt.* Kampala: Makerere University Press.

Funk, E. R. (1997). “The Power of Naming.” imepatikana tarehe 21/11/2011.katika http/www feminist.com/arehizies/oln 4 male fom html.

Griffen, E. M. (1997). *Afirst look at Communication Theory.*New York: Mc, Graw Hill. Campanies Inc.

Guma, M. (2001). “The Culture Meaning of Name among Basotho of Southern Africa: A Historical and Linguistic Analysis.” Katika, *Nordic Journal of African Studies 10 (3); 265-279.*

Hymes, D. (1964). *Language and Culture and Society.* New York: Harper and Row.

Halima, J. (2010). “Dhana ya Magofu ya Watawala wa Jadi.” Tasinifu ya Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Ibrahim, H. N. (2010). *Majanalisation of Muslim and the State in Tanzania*. Dar es Salaam: AERA

Kagenge, M. (2001). *English for Tanzania Secondary School.* Dares salaam: Afrophus Industries LTD.

Kombo, D. K. na Trump, D. L. (2006). *Proposal and Thesis Writing Nairobi:* Pauline Publications Africa.

Kothar, C. R. (2004). *Research Methodology: Method and Technigues, Second Revised Edition*. New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Msanjila, Y. P, Kihore, Y. & Massamba, D. B. P. (2009). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo.*Taasisi ya uchaguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu Dares salaam.

Mulokozi, M. M. (1983). "Utafiti wa Fasihi Simulizi." Katika *Makala ya Semina za Kitaifa.* Dar es Salaam: TUKI.

Mzee, S. Y. (2014). "Nafasi ya Majina ya Mizimu na Pepo za Makunduchi katika Kuhifadhi

Utamaduni wa Makunduchi." Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro Tanzania (haijachapishwa).

Mdee, S. J. & Mwansoko, H. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21: Kamusi ya Kiswahili yenye Uketo zaidi katika Karne hii*. Nairobi: Longhorn Publisher LTD.

Majapela, P. (2009). "Namna Ngeli zinvyosaidia Kuunda Majina ya Watu." Dissertation University of Dar es Salaam.

Neuman, W. I. (1991). *Social Research Methods*. U. S.A: Ally and Bacon. A Division of Simon and Schuster, Inc.

Njozi, H. M. (2010). *Muslim and the State in Tanzania*. Dar es Salaam: DUMT.

Roden, D. (1974). "Some Geographical Implication from the Study of Ugandan Place name." In *East African Geograghical Review vol. 12pp (77-86).*

Schotsman, P. (2003). *Place Names in Dar es salaam Tanzania*. Netherland: Laiden University.

Seif, D. G. (2011). *Nyimbo za Jando katika jamii ya Kikaguru, Kata y a Gairo.* Tasnifu ya M.A Kisawhili Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y (2009). *Fasihi za Kinchi.* Dar es Salaam: *AERA.*

TUKI (1990). *Kamusi ya Isimu na Lugha.* Dar es Salaam: Education Publishers and Distributors.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

Wamitilia, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi:Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi Phonix Publishers.

Wamitilia, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Zubeir, Z. S. (2015). “Etimolojia ya majina ya Kaskazini Pemba kuwa Utambulisho wa Utamaduni wa Wapemba.” Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATISHO I: MTAFITI AKIHOJIANA NA BAADHI YA WATAFITIWA



Mtafiti (kushotoni) akihojiana na mtafitiwa katika mtaa wa Mwembemajogoo tarehe 09/01/2018 saa 5.00 asubuhi.



Mtafiti (kuliani) akihojiana na mtafitiwa katika mtaa wa Mwembepunda tarehe 17/01/2018 majira ya saa 10.00 jioni.

**KIAMBATANISHO II: MUONGOZO WA MASWALI YA HOJAJI**

Hojaji hii ni kwa ajili ya utafiti wa "Majina ya wanyama ndege na wadudu jinsi yanavyoakisiwa na majina ya mitaa" Tafadhali unaombwa ujibu maswali yafuatayo kwa mujibu wa uelewa wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa mchango na matokeo yatakayosaidia kuleta mafanikio katika lugha ya Kiswahili pamoja na utamduni wa Mswahili.

Majibu yatakayopatikana yatatumika kwa ajili ya taaluma na yatakuwa siri baina ya mtafiti na watafitiwa.

A) TAARIFA ZA MTAFITIWA

Weka alama ya vyema (√) mahala panapo husika.

Umri ……………..

Jinsia Mke [ ] Mume [ ]

Kijiji unachoishi…………………….Mkoa……………………………….

Wilaya ………………………………Kiwango cha elimu …………………….

Kazi……………………………………..

B) MASWALI YA HOJAJI

1. a) Je ni mzaliwa na mkaazi wa kijiji ulicho kitaja hapo juu?

   Ndio [ ] Hapana [ ]

b) Kama jawabu lako ni ndio. Andika historia ama elezea utamaduni uliotumika katika kuibua jina la mtaa unaoishi.

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

2. a) Je kuna sababu zozote za kijamii ambazo zimepelekea kuibuka kwa jina hilo? Ndio [ ] Hapana [ ]

b) Kama jibu lako ni ndio. Elezea sababu hizo

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………

3. a) Je unafikiria utoaji wa majina kwa kuzingatia itikadi na umashuhuri / umaarufu unakidhi haja?

   Ndio [ ] Hapana [ ]

   b) Kama jawabu ni ndio taja umuhimu mitatu ya utoaji wa majina kwa kuzingatia itikadi na umaarufu /umashuhuri.

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………….

4. a) Je kuna vigezo vyovyote vya kimazingira ambayo vimepelekea kuibua jina la mtaa unaoishi?

   Ndio [ ] Hapana [ ]

   b) Kama ndio taja vigezo hivyo.

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………

   …………………………………………………………………

5. Taja vigezo vyengine ambavyo hupelekea kuibua majina ya mitaa

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

…………………………………………………

6. Toa mapendekezo yako juu ya utoaji wa majina ya mitaa

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

7. Majina ya mitaa yana miundo tofauti ya lugha. Kuna iliyo na majina ya miti,wanyama, muambatano wa majina,sitiari, ndege na wadudu,

a) Orodhesha majina matatu ya mitaa yenye asili ya majina ya wanyama, na ueleze kwa

nini mitaa hiyo ikaitwa jina hilo.

i)......................................................................

ii)......................................................................

iii)........................................................................

b) Taja majina matatu ya mitaa yenye asili ya majina ya ndege na ueleze kwa nini ikaitwa majina hayo

i. ……………………………………………………………………….

ii. ………………………………………………………………………..

iii. ………………………………………………………………………

c) Taja majina matatu ya mitaa yenye asili ya majina ya wadudu na ueleze kwa nini ikaitwa majina hayo.

i. ………………………………………………………………

ii. …………………………………………………………………….

iii. ……………………………………………………………………

AHSANTE SANA KWA USHIRIKIANO WAKO

**OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA**

P.O. Box 23409
Dar es Salaam, Tanzania
http://www.out.ac.tz

Tel: 255-22-2666752/2668445 Ext.2101
Fax: 255-22-2668759
E-mail: drps@out.ac.tz

**21/08/2018**

**SECOND VICE PRESSIDENT**
**P.O BOX 239,**
**ZANZIBAR.**

**RE: RESEARCH CLEARANCE**

The Open University of Tanzania was established by an act of Parliament no. 17 of 1992. The act became operational on the 1st March 1993 by public notes No. 55 in the official Gazette. Act number 7 of 1992 has now been replaced by the Open University of Tanzania charter which is in line the university act of 2005. The charter became operational on 1st January 2007. One of the mission objectives of the university is to generate and apply knowledge through research. For this reason staff and students undertake research activities from time to time.

To facilitate the research function, the vice chancellor of the Open University of Tanzania was empowered to issue a research clearance to both staff and students of the university on behalf of the government of Tanzania and the Tanzania Commission of Science and Technology.

The purpose of this letter is to introduce to you **Mrs MWAKA MZEE MOHAMMED PG201610607** who is a Master student at the Open University of Tanzania. By this letter, Mrs MWAKA MZEE MOHAMMED has been granted clearance to conduct research in the country. The title of her research is "**- MAJINA YA WANYAMA,NDEGE NA WADUDU YANAVYOAKISIWA NA MAJINA YA MITAA**".

The research will be conducted in Zanzibar commission of tourism. The period which this permission has been granted is from 03/01/ 2018 to 10/02/2018.

In case you need any further information, please contact: The Deputy Vice Chancellor (Academic); The Open University of Tanzania; P.O. Box 23409; Dar es Salaam. Tel: 022-2-2668820 we thank you in advance for your cooperation and facilitation of this research activity.

Yours sincerely,

OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA
P.O. Box 2599
ZANZIBAR
ZANZIBAR COORDINATION CENTRE

DRC: ZANZIBAR

For: VICE CHANCELLOR